ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32 Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kwanza – Tarehe 13 Juni, 2012

Kikao Kilianza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi

DUA

Mhe. Spika (*Pandu Ameir Kicho)* alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama mnavyoelewa kwamba katika Mkutano uliopita tulikuwa na kazi kubwa ambayo Baraza hili liliifanya. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 28 Machi 2012 hadi tarehe 22 Aprili 2012 Baraza lilipitisha Miswada saba ya Sheria kama ifuatavyo.

(1) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 ya Mwaka 1996 na Kutunga Sheria Mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

(2) Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya mwaka 1989 na Kutunga Sheria Mpya kwa Ajili ya Uendeshaji wa Tume ya Mipango Zanzibar, Kazi Zake, Uwezo Wake na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo.

(3) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

(4) Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 5 ya Mwaka 2012.

(5) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

(6) Mswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Utalii Nam. 6 ya Mwaka 2009

(7) Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Na huu ndio Mswada wa mwisho.

Kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 90(3) cha Kanuni Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2011 naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo sasa imekuwa ni sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa Wajumbe hiyo ndiyo kazi nzuri mliyoifanya, nawapongeza sana kwa kazi nzuri na Mhe. Rais ameikubali. Ahsante sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani, nakala zote za gazeti rasmi la serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 21 Aprili 2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mezani Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, lakini kabla sijaiwasilisha Mhe. Spika, naomba kwanza niseme yafuatayo.

Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujualia kuwa wazima na wenye afya. Pili napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuiweka sheria hii ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83. Tole la Mwaka 2012 toleo lililobadilishwa mwaka 2012 hapa Mezani.

Mhe. Spika, kabla sijafanya hivyo naomba uniruhusu kwa faida ya Baraza lako tukufu na kwa faida ya wananchi wote kwa ujumla niseme yafuatayo:

Mhe. Spika, chimbuko la Sheria hii ni pale ambapo Mswada wake kwa mara ya mwanzo uliletwa Zanzibar na kufanyiwa *public hearing* tarehe 18 na 19 Novemba mwaka jana 2011 hapo Bwawani na Skuli ya Haile-Selassie. Baada ya hapo Mhe. Spika, Mswada ulirejeshwa Bungeni kwa mazingatio ya maoni yaliyotolewa na Wazanzibari. Baada ya marekebisho hayo Mswada ulijadiliwa tena, na Waheshimiwa Wawakilishi wakapata semina kwa kujadili zaidi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi kwani maoni yao na mapendekezo yao ya busara yakazidi kuuweka Mswada huo vizuri na sasa ukachukua sura halisi ya Muungano. Kila upande wa muungano ulikuwa na haki na fursa sawa.

Mhe. Spika, mambo muhimu kama vile uhalali wa kujadili Muungano wetu, kama ilivyo katika kifungu cha 9.3 cha sheria hii. Marais wawili wote washauriane na wakubaliane kama ilivyo kifungu cha 5, 6, 20(1) na 20(3) cha sheria hii. Wajumbe wa Tume kwa idadi sawa kutoka kwa pande zote mbili za Muungano, kama ilivyo kifungu cha 13(5). Kuwa na idadi sawa ya Wajumbe wa Tume kama ilivyo kifungu cha 6.2.

Mwenyekiti na Katibu na Naibu Katibu wateuliwe kwa uwiano wa pande zote mbili za muungano, kama ilivyo kifungu cha 7(2) na 13 (2) kuhakikisha kuwa Bunge la Katiba lina Wawakilishi wa pande zote mbili za Muungano kikamilifu bila ya uonevu wowote ule kama ilivyo kifungu cha 22(1)(a) na (b) na kifungu cha 22(2).

Mwenyekiti na Makamo wake, Katibu na Naibu wake, wateuliwe kwa uwiano kama ilivyo kifungu cha 23(1), 23(2) na 24(1) na 24(2). Utaratibu wa upigaji kura ni kwa kila upande yaani Tanzania Bara na Zanzibar na ni lazima ufikie theluthi mbili kwa kila upande kama ilivyo kifungu cha 26(2). Katika kura ya maoni ya kupitisha katiba lazima Zanzibar kwa upande wake na Tanzania Bara kwa Upande wake. Kila mmoja wao akubali kwa zaidi ya asilimia 50 na mengineyo.

Mhe. Spika, haya ni baadhi tu ya mambo ambayo tulikubaliana na yote huwemo katika sheria hii mpya. Mhe. Spika, baada ya hapo Bunge likaupitisha Mswada huu kuwa sheria katika kikao chake cha Februari mwaka huu.

Mhe. Spika, naomba tukumbuke kuwa baada ya kuupitisha Mswada huo kuwa sheria, Mhe. Rais Kikwete alikutana na vyama mbali mbali vya siasa ikiwemo chama cha CUF, CCM, CHADEMA na kadhalika kuutafakari zaidi Mswada huo na walikubaliana kuufanyia marekebisho machache ambayo hayakuathiri hata kidogo maudhui ya sheria yote na ile hatua tuliyofikiwa ya kuwa sasa sheria hii ni kwa Zanzibar na Tanzania Bara.

Baada ya yote hayo kufanyika na kupitishwa na Bunge, sheria hatukuweza kuileta katika Baraza lako la Wawakilishi Mhe. Spika, katika kikao cha Machi/Aprili kwa sababu zifuatazo.

- Utaratibu wa kutia saini kwa Mhe. Rais Jakaya bado ulikuwa haujakamilika. Hii ni kwa sababu Mswada kwanza ni lazima upelekwe tena kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuupitia tena. Baada ya hapo ni lazima upelekwe kwa katibu wa Bunge ili na yeye aupitie na halafu atie saini yake na baadae aupeleke kwa Mhe. Rais kwa kuukubali.
- Baada ya hayo kumalizika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha Machi/Aprili kilikuwa kimeshamalizika. Kikao chengine kinachofuata ndicho hichi tunachokianza leo. Hii ndio sababu kwa nini sheria hii tukaileta mezani hii leo.

Mhe. Spika, kifungu cha 132(2) cha Katiba ya Zanzibar kinasema hivi:-

> "Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa inatumika kwa Tanzania nzima, basi sheria kama hiyo ni lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika"

Mhe. Spika, kupelekwa mbele ya Baraza maana yake ni kuweka hati hiyo Mezani, ni kwa Madhumuni ya Waheshimiwa Wawakilishi wapate taarifa ya jambo husika. Kwa mfano Bunge la Uingereza walilitafsiri neno hili kuingia hata pale inapowasilishwa hati inayohusika Afisini kwa Katibu tu na baadaye Katibu akazigawa kwa Wajumbe wake. Lengo kubwa ni kupata taarifa kwa wajumbe. Hichi ndicho kiini cha kifungu cha 132(2) ambacho kilitiwa kwa makusudi na waandishi wa Katiba ya Zanzibar waliokusudia kuliondoa tatizo lile lililokuwepo la Tanzania Bara kutunga sheria za Muungano bila hata upande wa pili wa muungano kujua kuna nini.

Mhe. Spika, la pili muhimu ni kuelewa kujua kuwa Baraza la Wawakilishi halina mamlaka hata kidogo ya kujadili masuala yanayohusu muungano. Hayo ni mamlaka ya Bunge la Jamhuri kama kifungu cha 64(3) cha Katiba ya Jamuhuri ya Muungano kinavyotaka.

Mhe. Spika, kwa sababu hizo, Baraza la Wawakilishi kinachotakiwa ni kupewa taarifa hiyo bila ya kujadiliwa, kwa sababu Baraza la Wawakilishi halina mamlaka ya kujadili. Hata ikiwa itajadiliwa Bunge halimiliki kuchukua maoni ya chombo chengine chochote.

Mhe. Spika, hivi karibuni Mahakama ya Rufaa ilitoa uamuzi wa mapendekezo na maelekezo katika kesi muhimu ya Seif Sharif Hamad ambapo iliamuliwa kuwa sio lazima kwa sheria za muungano kufanya kazi Zanzibar, basi sio lazima kwanza ziwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi. Bunge lina mamlaka pekee katika suala hili, ikiwa sheria hiyo ni mambo ya muungano. Na ikiwa imepitishwa kihalali katika Bunge basi sheria hiyo itatumika mara moja.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo na maelezo ya vifungu vya Katiba zote mbili suala la kujadili sheria iliyopitishwa na Bunge la Muungano haliwezi kufanywa kisheria katika Baraza la Wawakilishi. Kutokana na yote hayo sheria hii hatukuicheleweshe kuipeleka katika Baraza lako tukufu, na kikao hichi ndicho kikao pekee na cha kwanza ambacho kimekutana baada ya taratibu zote za sheria ile kukamilika.

Mhe. Spika, naomba nitumie nafasi hii ya Kikatiba niliyonayo chini ya kifungu 132(2) kusema rasmi kuwa Sheria hii ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83. Toleo la Mwaka 2012, iliyotungwa na Bunge la Jamuhuri ya Muungano sasa naiwasilisha Barazani. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Katiba na Sheria. Naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pili tuzishukuru serikali zetu zote mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya suala la Mswada ambao umewekwa Mezani hivi punde.

Jambo hili limepata upana wa mazingatio kutoka kwa wananchi, kutoka kwa wajumbe ambao ni sisi hapa. Lakini hatimaye serikali zote mbili zimekaa kwa pamoja kufikiria kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Katiba, na Sheria. Hatimaye tukashiriki kikamilifu kupitia kwa Waziri wa Katiba na Sheria kwenda katika Kamati ya Bunge kuhakikisha maoni ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi yanaingia katika Mswada, ambao hatimaye hivi sasa umekuwa sheria rasmi iliyopitishwa na Bunge. Nadhani msingi huu uwe ndio msingi wa mambo mengine yote ambayo yanatungiwa sheria za kutumika kwa pande zote mbili za muungano. Msingi wake upate mawazo ya pande zote mbili za muungano kutoka serikalini, kutoka kwa wajumbe kama tulivyotoa maoni kwenye Mswada huu. Hii itakuwa inatuwekea msingi madhubuti sana juu ya mambo yetu yanayohusu muungano kwa maslahi ya muungano wenyewe, lakini pia na kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania wote. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi(OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuweka Mezani hotuba ya kuwasilisha mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 30

Vitambulisho vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imo mbioni kutoa vitambulisho vya Uraia nchi nzima. Na kwa kuwa Zanzibar ambayo ni upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano tayari imeshatoa kwa wananchi wake vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi. Na kwa kuwa taarifa zinazohitajika katika vitambulisho vya Jamhuri katika zote ni zile zile zilizomo kwa vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi.

Je, kwa Wazanzibari ambao tayari wana vitambulisho vya Mzanzibari (ZAN ID) kuna ulazima gani wa kuchukua tena ID za Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 30 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vimetolewa chini ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, na inampa kila Mzanzibari mwenye sifa ya ukaazi kuwa na kitambulisho hicho.

Mhe. Spika, vitambulisho vya Taifa vitakavyotolewa kuzingatia sheria iliyotungwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano itamlazimu kila Mtanzania kupata kitambulisho ambacho kitatolewa na Mamlaka ya vitambulisho vya taifa NIDA, kwa ajili ya kumtambua Mtanzania kwa uraia wake na utaifa wake.

Mhe. Spika, kwa kuwa kila Mzanzibari ni Mtanzania basi Wazanzibari wenye vitambulisho vya ukaazi wanapaswa kuwa na vitambulisho vya Taifa vya Tanzania bila ya kuathiri Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 ambayo ni kwa ajili ya Wazanzibari tu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza suali dogo la nyongeza.

(1) Mhe. Spika, kwa kuwa tangu zamani, sasa na hata baadaye, Wazanzibari wanaamini kwamba Uzanzibari kuliko Utanzania. Na kwa kuwa kuna Wazanzibari wengi walionyimwa vitambulisho vya Uzanzibari ukaazi kwa sababu za hapa na pale zisizokuwa za msingi. Je, isingekuwa vyema kwa hawa walionyimwa vitambulisho vya Uzanzibari ukaazi wakapewa kwanza hivi vya Uzanzibari Ukaazi baadaye ndio vikafuata hivyo vya Tanzania.

(2) Kwa kuwa Baraza lililopita juzi tu hapa, tulipata ushahidi kuwa kuna watu wasiokuwa Watanzania ambao wamepewa vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi na kuchukua haki za Wazanzibari kama vile ajira na mambo mengine kadhaa wa kadhaa. Je, ni lini serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya Umoja wa Kitaifa ifatanya utafiti wa kina na upembuzi yakinifu na kuwanyang'anya vitambulisho wale wote waliokuwa sio Wazanzibari na hatimaye wale wazanzibari wakapatiwa vitambulisho hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika,

(1) Nakubaliana naye kwamba Uzanzibari mwanzo ndio baadaye unakuwa Mtanzania. Kwa sababu tumezaliwa Tanzania ndio baadae unakuwa Mtanzania kwa mujibu wa sheria yetu. Kwa hivyo Uzanzibari siku zote unalindwa na Utanzania siku zote utalindwa.

(2) Kuhusu wananchi wengine ambao wana haki ya kupewa vitambulisho vyao na mpaka sasa hawajapewa vitambulishyo vyao. Hilo ni kosa, lazima kila mwenye haki apewe haki yake na kitambulisho chake cha Mzanzibari apate.

Kwa hivyo suala hili linashughulikiwa na wahusika na wale wote ambao hawajapata vitambulisho vyao waende kwa Ofisi husika waombe na ikitokea kwamba wanasumbuliwa na hawapewi, nakuomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane unipe taarifa hizi ili serikali ichukue hatua zaidi.
Kwa wale ambao si watanzania kwa maana hiyo hawana sifa ya kuwa Wazanzibari, na wakapewa vitambulisho hivyo hivi sasa kuna zoezi maalum la kutafuta wale ambao hawana haki ya kuwa Wazanzibari na wanavyo vitambulisho hivyo, hatua za kisheria zitachukuliwa. Hatua kali kwa wale ambao wametoa vitambulisho hivyo vile vile zitachukuliwa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi nimuulize Mhe. Waziri suali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi yetu sasa hivi imo katika taratibu za marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Na kwa kuwa ndani ya Muungano huu Tanzania ni Taifa moja, lakini kwa kuwa uwezekano wa kuja kutokea taifa zaidi ya moja upo. Mhe. Waziri haoni kuna haja sasa kwa Wazanzibari kwanza kusitishiwa zoezi hili la kupewa vitambulisho vya Taifa la Tanzania mpaka hapo mchakato wa Katiba utakapomalizika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, mchakato wa katiba ni suala mbali, na haki ya Mtanzania kupata kitambulisho chake ni suala mbali, na haki ya Mzanzibari kupata kitambulisho chake ni suala mbali. Ni vyema kabisa Wazanzibari wakapata vitambulisho vyao. Kwa sababu muungano huu sisi ni

wadau, usingekuwepo kama hakuna Zanzibar na Tanganyika. Kwa vyovyote tuna haki zetu ndani ya muungano. Kwa vile haki zetu tuzipate na hata litakapotokea jengine lolote basi hizi haki za sasa hivi ni lazima tuzipate.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii. Kwa nia njema kabisa ile Kamati inayotoa vitambulisho vya Jamhuri ya Muungano iliandaa utaratibu wa kutoa hata maskulini. Kwa kuwa naamini kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haina hitilafu na vijana wake wanaosoma. Kwa nini utaratibu huu Zanzibar haujachukua na vijana wetu wanamaliza skuli hawana vitambulisho wengi, wanakosa haki zao nyingi kabisa hata za kujiandikisha kwenye kufanya mitihani wanaulizwa zitambulisho kwa ajili ya kulipia. Ni kwa nini serikali haichukui hatua ikaanza utaratibu wa kuwatayarishia vitambulisho wanafunzi wetu walioko maskulini na vyuoni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kifupi halikuwa suali bali ulikuwa ni ushauri. Mimi naamini ni ushauri mzuri, tutaupokea tuufanyie kazi kwa mujibu wa taratibu za sheria zilizopo.

Nam. 2

Ujenzi Wa Uzio Kiwanja Cha Ndege Cha Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Katika hatua ya kuhifadhi na kuimarisha viwanja vya ndege vya Zanzibar, Mamlaka ya Uwanja wa Ndege imeamua kukijengea uzio kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume, Zanzibar (Abeid Amani Karume International Airport) kwa kutumia gharama kubwa sana huku taarifa za ujenzi huo zikiwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi mara kwa mara, pamoja na taarifa kwamba Mradi huo tayari umeshakamilika. Hata hivyo, hivi sasa kuna ujenzi wa uzio unaoendelea kujengwa, nje ya uzio uliopo sasa.

(a) Je, eneo linaloendelea kujengwa uzio huu wa pili, nje ya uzio wa awali linamilikiwa na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege.

(b) Ni sababu zipi zinazopelekea kujengwa kwa uzio mwengine nje ya uzio uliopo sasa.

(c) Ni kampuni gani inayojenga uzio huo na mpaka kukamilika kwake, utagharimu kiasi gani.

(d) Je, Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwamba, hali hii ya kujenga uzio mara mbili, inatokana na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kukosa mpango maalum (Master plan) wa kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 2 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d). kama ifuatayo:-

Mhe. Spika, taarifa za ujenzi zilizowasilishwa katika Baraza la Wawakilishi ni kamilifu zinahusiana na kukamilika kwa nusu ya mwanzo ya ujenzi wa uzio unaozunguka eneo lote la Uwanja wa Ndege lenye urefu wa kilomita 12.18.

Mhe. Spika, hivi sasa ujenzi unaoendelea ni kukamilisha nusu ya mwisho ya kilomita 6.3 zilizosalia.

(a) Mhe. Spika, eneo linaloendelea kujengwa la uzio hivi sasa linamilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa hati miliki No. 278/97 ya tarehe 23/09/1997.

(b) Sababu zilizopelekea kujengwa kwa uzio huo ni kuhakikisha kuwa Mamlaka inalidhibiti eneo lote lililotengwa na Serikali Kuu kwa ajili ya Maendeleo ya Uwanja wa Ndege kutokana na hati miliki ya mwaka 1997 kama tulivyoeleza.

(c) Kampuni inayojenga uzio huo ni Kampuni ya Sogea Satom kutoka Ufaransa na gharama za ujenzi huo ni shilingi bilioni sita, mia mbili arobaini na moja milioni, laki nane, elfu tano thamanini na mbili na senti arobaini na saba, kwa urefu huo wa kilomita 12.18.

(d) Ukweli ni kwamba, sehemu kubwa ya eneo lililotajwa hapo juu limevamiwa na wananchi kwa harakati za ujenzi na kilimo, ili kukamilisha ujenzi wa uzio katika eneo lote la uwanja, hatua ya kufanya

tathmini na kulipa fidia kwa watu wote ilihitajika, kitu ambacho kingepelekea utekelezaji wake kuwa ni mgumu kutokana na gharama kubwa ambayo ingejitokeza.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana ujenzi wa uzio wa mwanzo ulifanyika ili kuepusha gharama hizo zilizotarajiwa.

Mhe. Spika, hata hivyo kutokana na umuhimu wa kulidhibiti eneo lote la uwanja kwamujibu wa hati miliki ya mwaka 1997, ndio maana Serikali Kuu kwa makusudi iliamua kufanya mabadiliko ya ujenzi huo na hatua za ujenzi wa uzio wa pili unaoendelea hivi sasa zikaanza. Kwa hivi sasa kazi ya ujenzi katika eneo hilo inaendelea vizuri.

Baada ya kukamilika ujenzi huo, hatua za kuuondosha uzio uliojengwa hapo mwanzo, zitafanyika kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali la nyongeza. Mhe. Spika, katika hatua za ujenzi wa uzio kwenye eneo la Uwanja wa Ndege wamekuwepo wananchi ambao wamepata athari na wanahitaji fidia, miongoni mwa fidia hizo ni majengo pamoja na viwanja. Kumekuwepo na taarifa kwamba fidia hizo zimekuwa za upendeleo yaani wenye nyumba wanapewa pesa ndogo zaidi kuliko wenye viwanja.

Namuomba Mhe. Naibu Waziri atwambie hilo ni kweli.

Lakini pili amesema kwamba uzio huu unajengwa kwa shilingi bilioni 6.2 na Kampuni hiyo ya Sogea Satom. Je, ni kwa hii awamu ya pili tu au tangu mwanzo, kama ni kwa awamu ya pili tu je, ile awamu ya mwanzo ilikuwa shilingi ngapi.

Mwisho kwa nini kila mradi unaojengwa na kusimamiwa na wizara yake chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege umekuwa na mikosi ya kukwama. Kwa mfano, uliwahi kukwama Uwanja wa Ndege uliokuwa ukijengwa na Wachina, sasa hivi kuna taarifa kwamba *terminal* mpya inakwama na uzio unakwenda msobemsobe. Ni kwa nini hasa wizara yake inashindwa kusimamia miradi yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tunachokizungumza hapa ni suala la fidia inayohusiana na ujenzi wa ukuta. Suala alilioliuliza Mhe. Mwakilishi nadhani anakusudia eneo jengine lililo nje ya ukuta huu. Katika ukuta huu unaendelea kujengwa hivi sasa kulikuwa kuna nyumba chache sana, miongoni mwao ni nyumba ya Mzee Ali Mwinyichande, wengi wa watu ambao wamelipwa fidia katika ujenzi wa ukuta unaoendelea ni watu ambao walikuwa na miti na vipando na tayari serikali katika awamu ya kwanza imeshalipa fidia kwa takriban zaidi ya shilingi milioni mia mbili na arobaini na moja kwa watu hao ambao walikuwa na vipando katika eneo hilo ili kupisha ujenzi huo wa ukuta.

Awamu ya pili ya watu ambao ukuta haujajengwa ikiwa kuna kila mtu anayestahili kulipwa fidia serikali itafanya hivyo kabla ya kuendeleza ujenzi wa ukuta ule.

Suala la pili Mhe. Spika, suala la gharama tumeshaeleza kwamba jumla ya gharama ni shilingi bilioni sita, kazi ambayo wameifanya Sogea Satom ina-*worth* shilingi 3.2 bilioni, tulichomlipa serikali ni shilingi 2.6 bilioni bado anatudai shilingi 600 milioni kukamilisha kazi.

Lakini Mhe. Spika, jambo la kutia moyo ni kwamba mjenzi huyu amejenga imani na mapenzi na bado ameonesha nia ya kuendelea kutusaidia kujenga na ataendelea kutudai na tutamlipa kila hali inaporuhusu.

Mhe. Spika, swali lake la tatu mimi siamini kwamba kuna miradi ambayo inaendeshwa na Uwanja wa Ndege inakwama kwa sababu ya uzembe, kama kuna mradi ambao utakuwa umekwama unaosimamiwa na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege utatokana na sababu za msingi na Serikali Kuu itakuwa inazifahamu. Mradi uliopo wa Uwanja wa Ndege sasa hivi wa jengo haujakwama ni utaratibu wa mkataba kama tunavyotambua kwamba mkataba wa jengo lile ulikuwa uko wazi unaeleza kwamba jukumu la mjenzi ata-*design*, jukumu la mjengewa (serikali) ata-*prove* michoro baada ya kujiridhisha ndio michoro iéndele. Kwa hivyo, kilichopo mjenzi ametuletea sisi serikali, tumeipitia muda wote tulikuwa hatujaridhika na baada ya kujiridhisha serikali tumemruhusu na ujenzi wa jengo lile unaendelea.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuwa kwa pamoja kwa mintarafu ya kupitisha mambo mbali mbali ya taifa letu. Lakini pia nichukue nafasi hii nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi.

Sasa naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu marefu na mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Je, atakubaliana na mimi kwamba kweli uzio wa pili uliojengwa ni kwamba pamoja na maswali aliyouliza Mhe. Hija Hassan kuwa hii inaonekana si utaratibu mzuri na walikuwa hawajui kwamba lile eneo lao la uzio ni eneo gani la Uwanja wa Ndege ili kugharimu fedha nyengine zaidi Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, historia inavyoeleza Uwanja wa Ndege wa Kisauni umeasisiwa mwaka 1956, kwa wakati huo uwanja ule ulikuwa uko nje ya mji. Kwa kutambua kipindi kinachopita na maendeleo yanavyotokea katika nchi, ndio mwaka 1997 serikali ikafanya maamuzi ya msingi ya kutenga eneo kubwa kwa ajili ya maendeleo ya Uwanja wa Ndege. Lakini naomba Mhe. Spika, sote tukiri kwamba serikali tulifanya uzembe mkubwa sana, tuliwaruhusu wananchi wetu kuvamia eneo la Uwanja wa Ndege kwa majenzi pamoja na vipando na hali hiyo ndio iliyopelekea usumbufu huo unaojitokeza hivi sasa.

Mhe. Spika, ukiichukua hati ya Uwanja wa Ndege ya mwaka 1997 eneo ambalo wana-*cover* chini ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ni eneo kuwba sana, limepakana na upande wa Jeshi kwa upande wa Kusini Magharibi. Ni imani yangu kwamba nyumba za wananchi hizo tunazozipigia kelele ni nyingi zaidi na hapo ndipo serikali ilipofanya tafakari kwa kuona kwamba hatua ya kwanza tuzuie ili tuendane sambamba na mradi wa *Runway* ambao walipendekeza *World Bank* kwamba ni vyema tunapojenga *runway* muandae na uzio.

Hatua ya kwanza Mhe. Spika, ndio uzio ule ukajengwa kwa ndani, lakini baada ya kuona tathmini kwamba bado wananchi wanaendelea kuvamia ndio serikali ikafanya maamuzi ya kuongeza eneo lake na bado eneo hili lililojengwa uzio liko ndani ya eneo la mwaka 1997 hatujakiuka wala hatujalifikia na mimi imani yangu kwamba kama serikali itakuwa na fedha za ziada za kulipa fidia tuna haki ya kulichukua eneo lote la mwaka 1997, lakini sidhani kwamba ujenzi ule unaoendelea sasa hivi kama kuna gharama inayoingia serikali zaidi ya hiyo kuondoa huo usumbufu wa wananchi wetu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru na mimi kunipa nafasi hii na nimshukuru Mwenyezi Mungu kutuweka wazima mpaka sasa hivi. Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri na ufafanuzi mzuri aliyoutoa na ninaamini majibu mengine atakuja kutusaidia wakati wa bajeti yake vile vile.

Mhe. Spika, naomba nimuulize swali la nyongeza. Katika suala la msingi Mhe. Mwakilishi aliuliza suala zima la kujengwa ukuta wa mara ya pili katika eneo la Uwanja wa Ndege. Tunashukuru katika jawabu zake alieleza zitatumika kama shilingi bilioni sita Ambapo mpaka sasa hivi serikali imeshamlipa mjenzi shilingi bilioni mbili na yeye ameshatumia gharama kama ya shilingi bilioni tatu.

Kwa kuwa umejengwa ukuta wa mwanzo kwa gharama kubwa na sasa hivi kuna ukuta mwengine unajengwa na inaonesha ukuta ule hautoendana sambamba na ule ukuta wa Mwanzo; je, baada ya kujengwa huu ukuta wa pili kumalizika ule wa Mwanzo utavunjwa au utakuweko ndani, kama utavunjwa je, serikali itapata hasara kiasi gani.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Naibu Waziri kwa ufafanuzi mzuri tu katika maswali yote ambayo ameyajibu. Mhe. Spika, hakuna ukuta wa mwanzo na wa pili ni awamu ya ujenzi wa ukuta huo, umejengwa kwa awamu ya kwanza na sasa unajengwa kwa awamu ya pili. Kwa hivyo, sio kwamba kuna ukuta baadae utavunjwa, hakuna ukuta utakaovunjwa.

Lakini nieleze vizuri zaidi, ukuta ambao unajengwa tangu awamu ya kwanza na hii ya pili ni ukuta ambao hata ukitaka kuusogeza basi utafanya hivyo kirahisi mno. Kama wanaopita wanaona ukuta unavyojengwa ni kwamba kunawekwa nguzo halafu kunachukuliwa pande la zege linawekwa kwenye *slots*, pande hilo siku yoyote ukitaka kuliondoa unalichukua tu unaliweka mahali pengine ambapo unataka. Kwa hivyo, pamoja na ujenzi huo unavyoendelea hakuna ukuta utakaovunjwa kwa sababu ulijengwa vibaya au mahali sipo.

Hivyo Mhe. Spika, si suala la kwamba serikali itapata gharama ni ujenzi unaendelea awamu ya kwanza imemalizika na awamu ya pili na pengine kuwe na awamu ya tatu na ya nne kwa sababu ukuta ni mrefu na tunajenga kwa mujibu wa uwezo wetu tunapoupata. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 33

Uchimbaji Kokoto Wawi na Micheweni

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la serikali ni kuwawezesha wananchi kuongeza kipato akinamama wa maeneo ya Mashariki ya Kisiwa cha Pemba kama wale wanaoishi Vitongoji katika Jimbo la Wawi na Micheweni katika Jimbo la Micheweni wameekeza maisha yao kwa uchimbaji wa kokoto kwa kutumia mikono na nyundo.

Je, ni lini serikali itawawezesha wananchi hawa kwa kuwakusanya pamoja na hatimaye kuwapatia mashine (CRUSH) kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa lengo la serikali kupitia wizara yangu ni kuwawezesha kiuchumi wananchi wa Zanzíbar hasa akinamama na vijana, wote wenye uwezo wa kufanya kazi kwa kuongeza kipato, wizara yangu kwa kupitia Idara ya Ushirika imeshaanza kuwashajihisha na kuwakusanya pamoja wananchi wa jimbo la Wawi na Micheweni kwenye ukanda wa Mashariki ya Kisiwa cha Pemba ili kuanzisha vyama vya ushirika. Napenda kukuarifu kuwa vyama vya ushirika 45 vimesajiliwa vyenye wanachama 1,008 na vinafanya shughuli mbali mbali za kiuchumi zikiwemo upandaji wa mwani, miti na kilimo cha migomba.

Aidha, kwa vile miongoni mwa shughuli za wizara ni kutoa huduma na ushauri, wizara itakaa na wananchi hao ili kuona mahitaji, vifaa na zana wanazozihitaji ili kuwaunganisha na taasisi za kifedha kwa kuwapatia mikopo itakayowawezesha kununua mashine husika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa rasilimali mawe hupatikana kirahisi sana katika ukanda wa mashariki wa Kisiwa cha Pemba kwa mfano Vitongoji, Micheweni na hata Mwambe, na kwa kuwa wanawake wamewekeza katika kuvunja kokoto kazi ambayo ni ngumu mno lakini wanafanya hivyo kutokana na umasikini, na kwa vile unapomuwezesha mwanamke umeiwezesha jamii pamoja na familia.

Je, Mhe. Waziri ni lini ofisi yake itawakomboa wanawake wa Vitongoji, Wawi, Mwambe kwa kuwapatia njia mbadala za kujipatia *income generating* ukiangalia hii ya kuvunja mawe ambayo ni ngumu mno na hata hivyo vikundi vya ushirika alivyoanzisha naweza kusema ni *static and is not dynamic*.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwanza naomba nikubaliane naye kwamba kazi ya kubanja kokoto au kupasua mawe ni kazi ngumu. Lakini pia kwa upande mmoja na suala la mazingira pia linachangia katika kuharibu maeneo hayo.

Suala hilo hilo la kokoto pia kwa tafiti zilizofanywa zinawashirikisha hata watoto wadogo katika kutafuta njia za kupata riziki zao. Juzi nimetoa taarifa kwenye vyombo vya habarí kupiga marufuku utumiaji wa watoto katika shughuli za kazi kama hizo ambazo kwa kweli zinawadhalilisha na zinawaumiza. Sasa serikali kwa upande wetu tumeshakaa tayari na kama nilivyosema kwenye jibu mama nitafika kwenye eneo hilo tukae tushauriane ili kuwashauri wajiunge kwenye *SACCOS* ambazo zitaleta tija zaidi kuliko zile amabazo zitaumiza maisha yao na miili yao.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa azma ya serikali ni kuwakusanya wananchi na kuwasaidia kiuchumi, na kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwa tayari kuna vikundi vya Micheweni, Mwambe na Vitongoji; napenda kumuuliza kwanza. Je, katika vikundi hivyo ambavyo tayati tumevishajiisha na tayari vimejikusanya, serikali imewapatia kiasi gani cha fedha ili kuwainua kiuchumi.

Je, kwa kuwa tumewashajihisha wananchi na wameitikia wito huo, lakini kuna baadhi ya vikundi ambavyo tayari vimeshalipa fedha zao kwa ajili ya usajili na unakuwa mgumu usajili huo kuupata, kuna sababu zipi za msingi wananchi hao kuwa na ugumu wa kuwapatia usajili wa vikundi vyao.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwanza nampongeza sana kwa masuala haya ya kimsingi hasa hili la pili limekuwa mara nyingi likilalamikiwa suala la usajili. Naomba nianze na hili la pili kabla sijenda la Mwanzo.

Mhe. Spika, manung'uniko haya yanaletwa ni kweli lakini tatizo lililokuwepo ni ukamilishaji wa zile taratibu za usajili wenyewe, unapotaka usajili lazima upite kwenye njia maalum kuthibitisha, kwanza turidhike na hicho kikundi chako kwamba idadi ya wanachama imekamilika, kimepata baraka zote zinazohusika katika maeneo ambayo kinakaa kikundi kile, lakini usajili huwa hauzidi zaidi ya wiki moja kiutaratibu. Sasa namuomba Mheshimiwa kama bado tatizo hili linaendelea kwa sababu tumejitahidi sana kuliondoa hili tatizo, lakini baadhi ya wananchi wetu ukiwarejesha wanakwambia kwamba wizara imekataa kutusajili, inakataa kwa lengo la kwenda kurekebisha zile kasoro.

Sasa nitamuomba Mhe. Mwakilishi kama anayo idadi ya vikundi hivyo basi atuletee ili maafisa wetu walioko Pemba wende Micheweni mara moja kuwatafuta na kuwapatia usajili huo mara moja. Napenda kumhakikishia kwamba *Inshaallah* jambo hilo litatekelezwa haraka iwezekanavyo na wananchi wote wa maeneo mengine ambao vikundi vyao bado havijasajiliwa, kama kuna tatizo basi wafike pale ofisini tutachukua hatua za haraka kuvisajili.

Lengo la serikali kuvisajili vikundi vyote vya ushirika na ndivyo viitavyo-*qualify* kupata ile mikopo ambayo tutaanza kuitoa katika mwezi wa saba. Kwa sababu tayari hivi sasa serikali *Alhamdulillah* tumeanza utaratibu mzuri wa kukusanya fedha na hatutokuwa na tatizo la kifedha kiasi hicho katika kuwapatia mikopo wananchi wetu. Sirahisi kutaja kiwango cha fedha ambazo tutawapa au tutawapatia vikundi vile vya Mhe. Subeit Khamis, inategemea na ukubwa wa mradi wenyewe na yale mahitaji watatofautiana, kuna watakaopata shilingi milioni moja, milioni mbili au tatu. Kwa hivyo, kwa sasa hivi ni mapema kumwambia nitampa kiasi gani lakini akae mkao wa kuondoa umasikini.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia ruhusa hii asubuhi ya leo kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri mara nyingi sana mawaziri huwa wanatoa ahadi za kusema tutakwenda kuwatembelea wanavikundi. Je, Mhe. Waziri atatuahidi ni lini atakwenda kuwatembelea wananchi hao ili kuwaokoa wasiendelee kuumia mikono kwa kubanja hizo kokoto.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naomba alirejee swali hilo neno la mwisho sikulifahamu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nashukuru sana kwa kuwa suala zito nitaendelea kumuuliza Mhe. Waziri. Mara nyingi sana mawaziri huwa mnatoa ahadi za kutamka kuwa mtakwenda kuvitembelea vikundi au mtakwenda kwa wananchi kuhusu matatizo yao, lakini hatimaye mnakuwa hamwendi. Je, Mhe. Waziri ni lini atakwenda katika kikundi hicho ambacho kinabanja kokoto kwa mikono ili kuwanusuru wananchi wasiumie mikono.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, miongoni mwa mawaziri hao nadhani mimi sie, kwa hivyo nadhani mngekuwa wawazi zaidi nani hao ambao wanatoa ahadi za kwenda kutembelea watu halafu hawendi.

Lakini pili maeneo hayo mimi nimeshayatembelea Mhe. Spika, nimeshakwenda na tumekwenda mawaziri karibú wanne, si waziri mmoja tu ni mawaziri wanne. Mhe. Waziri wa Nchi, (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Waziri wa Habarí, Utamaduni, Utalii na Michezo na wengineo kuwataja itakuwa hatumalizi, na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Nam. 5

Kuvuja kwa Skuli ya Pale

Mhe. Mussa Ali Hassan - Aliuliza:-

Tunaipongeza serikali kwa kuwapatia elimu wananchi wake pamoja na kujenga majengo ya kisasa ya skuli za msingi na sekondari.

(a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kuwa skuli ya Pale inavuja.

(b) Kwa kuwa walimu wa skuli hii wanashindwa kufundisha hususan wakati wa mvua. Je, serikali ina mpango gani wa kuondosha tatizo hilo ili wanafunzi wa skuli hiyo waweze kusoma wakati wowote.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru sana na awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika hapa Wajumbe wako tukiwa wazima wenye afya njema na kuendeleza gurudumu letu.

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye vifungu (a) na (b), lakini kabla ya hapo Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikijenga majengo ya kisasa ya skuli za msingi na sekondari kwa lengo la kuwapatia nafasi za kusoma watoto wote wenye umri wa kwenda skuli. Lengo hili limekuwa likitekelezwa kwa ufanisi mkubwa kwa mashirikiano makubwa na wizara na washirika wa maendeleo katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu imemaliza jengo moja lenye vyumba viwili na ofisi moja katika skuli ya Pale kwa mwaka huu wa bajeti ambao tunamalizia.

(b) Wizara italifanyia ukarabati wa paa kwa jengo hilo kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu katika mwaka wa fedha wa 2012/13. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, ahsante sana nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba kujua ujenzi huu utaanza lini na kumalizika kabisa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali langu mama kuwa ujenzi huu utaanza mara tu bajeti yetu itakavyopitishwa na kadiri hali ya fedha zitakavyoingia. Kama nilivyozungumza mwaka huu ambao tumemaliza bajeti tumemjengea Mhe. Mussa jengo lake ambalo lina madarasa mawili na ofisi moja, haya majengo ni mengi, kuna yanayotaka matengenezo na yanayotaka kumalizwa. Kwa hivyo, kama nilivyozungumza Mwanzo kuwa katika mwaka huu jengo lake pia litajengwa lakini simwambii ni siku gani na mwezi gani ni kadiri hali ya fedha itavyoruhusu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabla sijauliza Mhe. Spika, naomba nihudhurishe masikitiko yangu makubwa sana kwa kusikia katika karne hii ambapo wanafunzi wetu wanajitayarisha kusoma kwa kompyuta majengo mengine yanavuja. Kwa hivyo, naomba nizifikishe salamu hizi kwa Mhe. Waziri ili aione hali hii.

Lakini swali langu la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nilivyoikumbuka mimi ilikuwa ina kitengo cha ujenzi maalum ambapo wanapitia skuli mbali mbali na kuona, inafikia vipi mpaka Mwakilishi analeta katika Baraza la Wawakilishi kuvuja kwa skuli na kitengo hiki kipo, kama kipo kinafanya kazi gani, na kama hakipo kwa nini kiliondolewa. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kitengo cha ujenzi cha Wizara ya Elimu bado kipo na kinafanya kazi zake kama kawaida, na mwakilishi kama ulivyo wajibu wake si vibaya kuuliza swali ili kuhimiza kwa sababu yeye ni msimamizi wa maendeleo katika jimbo ambalo anatoka. Tunajua skuli zetu zote ambazo zinavuja, tunajua majengo mangapi ambayo tayari tumekabidhiwa wizara tunayotaka tumalizie, kinachotukwaza Mhe. Spika, ni bajeti, bajeti ambayo tunapata ni ndogo.

Kwa mfano Mhe. Spika, mwaka huu bajeti ambayo tumeipata katika mradi huu wa kuendeleza elimu ya msingi, tulikuwa na bilioni 1 tu Mhe. Spika, wakati huo tuna majengo karibu 200 yanataka yamalizwe. Tuna majengo ambayo yanavuja sio kidogo. Kwa hivyo, sio kama hatufahamu au hiki kitengo hakifanyikazi. Kitengo kipo na kinafanyakazi na tunafahamu matatizo ambayo yapo katika skuli.

Lakini Mhe. Spika, katika hili mimi naomba nitowe wito kwa wananchi pamoja na wawakilishi ambao wamo humu Barazani. Kuna CDF ambapo wawakilishi wetu wanapewa, hebu wajaribu kuzipeleka hizi kwenye miradi hii ya elimu, kwa sababu jimbo moja wakati mwengine lina skuli karibu tatu au nne au tano, mzigo ambao tunao Wizara ya Elimu ni mkubwa. Kwa kushirikiana na kamati ya skuli na kamati zao za maendeleo basi wajaribu pesa hizi ambazo wanazipata watusaidie wasisubiri mpaka majengo haya ya mabunge.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la mwisho la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na rai aliyoitoa. Swali langu liko hapa.

Hivi mfuko huu wa jimbo unaotolewa pesa kidogo mwaka mara moja, je utaweza kweli kuhudumia ujenzi wa maskuli yote ambayo hayajaezekwa mpaka leo katika kila jimbo kwa mwaka mzima.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kupanga ni kuchagua, jambo lolote hata kwenye nyumba basi binadamu anakua na kipaumbele katika kufanya mambo yake. Kwa hivyo, hiki ambacho anahisi Mhe. Mwakilishi kinamkera na mimi nasema hakuna kitu kama elimu. Kwa sababu bila ya elimu hakuna maendeleo ambayo yatapatikana katika nchi yoyote.

Kwa hivyo, wao kama wawakilishi wakae watafakari ni kipi kipaumbele chao kwa mwaka huu kwa pesa ambazo wamepata, nakushukuru Mhe. Spika.

Nam. 11

Tatizo la Maji Mijini na Vijijini

Mhe. Ali Salum Ají - Aliuliza:-

Pamoja na jitihada kubwa na za muda mrefu zinazofanywa na Wizara katika kutatua tatizo la maji Mjini na Vijijini.

(a) Je, Mhe. Waziri ni mwaka gani hasa tatizo hili litapata ufumbuzi wa kudumu.

(b) Je, ni tatizo gani hasa linalopelekea tangi la SEMUSO Kibanda Maiti kutoingizwa maji na kuwaondoshea tatizo la maji wananchi wa eneo hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Wizara yangu kupitia mamlaka ya maji Zanzibar inaendelea na juhudi za kuwapatia wananchi wa mjini na vijijini huduma ya maji safi na salama kupitia miradi mbali mbali inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo pamoja na nguvu za ndani, juhudi hizo ni pamoja na kuibua miradi mipya ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya mijini pamoja na vijijini.

Mhe. Spika, kasoro iliyojitokeza ni kiwango kidogo cha umeme ambacho kinaifanya pampu ya kisima hicho kushindwa kusukuma maji kwenda kwenye tangi hilo. Tayari Mamlaka ya Maji inalishughulikia tatizo hilo na kuhakikisha inalipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba wakati wowote tatizo hilo litakapoondoka, basi wananchi wa Sebleni, Muungano, Sogea na Nyerere watafaidika na huduma hiyo ya maji safi na salama.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyonijibu, lakini pamoja na hayo naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la mradi wa SEMUSO ni la muda mrefu, yaani sio muda mrefu ni miaka mingi limekuwa ni tatizo sugu. Kila linapoulizwa swali basi jawabu linakuwa ndio hilo hilo kwamba wizara itajitahidi. Hebu Mhe. Naibu Waziri anihakikishie ni muda gani hasa wizara italiondosha tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli tatizo hili ni la muda mrefu, lakini nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba suala hili wizara yangu itajitahidi kuliondoa kwa kipindi kifupi, kwani hilo ndio lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuhakikisha kwamba vile vijiji vyote na miji ambayo ina matatizo ya maji kuyaondoa matatizo hayo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu mradi ule ulifadhiliwa na Serikali ya Marekani na kulikuwa na pampu kubwa ambayo ilikuweko pale na ikatolewa, nataka nijue hii pampu imepelekwa wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika.

(Hapa umeme ulizimika kwa muda mfupi)

Mhe. Spika: Umeme utarudi sasa hivi Mhe. Mjumbe endelea.

Baadhi ya Wajumbe: Hatuoni. *(Vicheko).*

(Baada ya dakika chache umeme ulirudi)

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza naomba nimjulishe Mhe. Mjumbe kwamba tatizo sio pampu, pampu iliopo kisimani ni nzuri sana, isipokuwa tatizo linalotusumbua ni tatizo linalosababishwa na umeme mdogo ambao unasababisha pampu hiyo kutokuwa na uwezo wa kupandisha maji kwenye tangi kutokana na nguvu ya umeme ambayo kwa sasa hivi iko katika hali ndogo.

Vile vile nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba suala hili tunalivalia njuga na tutajitahidi kuliondoa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa chimbuko la mradi huu wa maji wa SEMUSO tatizo lake la ukosefu wa maji liko katika shehia tatu, yaani Sebleni, Muungano na Sogea. Kwa kuwa mamilioni ya fedha za wahisani zimetumika na nguvu za wananchi pia zimetumika ili kuondosha matatizo hayo ya maji. Kwa kuwa inaonekana ni dhahiri kwamba Mamlaka ya Maji ZAWA imeutelekeza mradi huo kwa makusudi bila ya kujali nguvu za wahisani na nguvu za wananchi. Kwa kuwa katika bajeti hii nakusudia kuondosha shilingi ili kupata ufumbuzi zaidi wa tatizo hili.

Je, Mhe. Waziri utawaambia nini wananchi wa maeneo hayo ya Sebleni, Muungano na Sogea juu ya kuutelekeza mradi huo muhimu ambao umeanzishwa kwa gharama kubwa na hivi sasa haufanyi kazi na bado matatizo ya maji yanaendelea.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, mradi wa *SEMUSO ZAWA* hawakuutelekeza, kilichosababisha mradi wa *SEMUSO* kuwa na matatizo ni kwamba mradi huu kilipochimbwa kile kisima, lile eneo halikuwa na nyumba nyingi, kwa hivyo matumizi kwenye eneo lile yalikuwa ni madogo. Matokeo yake hivi sasa lile eneo nyumba nyingi zimeshamalizika na karibu kila nyumba imetia umeme, hivyo umeme katika eneo lile umezidiwa na kwa sababu hiyo umeme hauwezi kuifanya pampu kusukuma maji kupeleka kwenye tangi.

Mhe. Spika, nakumbuka kwamba ilipokuwa umeme mkubwa, basi kisima kile kilikuwa kikisukuma maji na kikipeleka kwenye tangi wakati huo kinachimbwa kile kisima. Lakini sasa hivi jitihada za kubadilisha waya za umeme katika maeneo hayo kwa mradi wetu wa *JICA* zinachukuliwa ili kuliondoa tatizo hili.

Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe asiwe na wasi wasi kwamba labda tangi lile litakaa pale kama ni *white elephant*. Tangi lile litafanyakazi na watu wa Sebleni, Muungano na Sogea watapata maji kama kawaida. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Spika: Anachosema Mhe. Waziri ni kwamba hiyo shilingi usije ukachukua. Haya nafikiri maswali tumemaliza na shughuli iliopo ni shughuli ya jioni. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi kinachotutaka kuanza Baraza saa 3:00 kamili za asubuhi mpaka saa 7:00 mchana na kuendelea tena saa 11:00 mpaka saa 1:45 usiku. Mhe. Spika, kwa kuwa leo ni siku maalum sio tu kwa Baraza la Wawakilishi bali pia kwa Zanzibar kwa jumla. Siku ambayo Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo atasoma bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa kuwa tumejiwekea utamaduni wa kusoma bajeti yetu mbele ya Baraza lako tukufu saa 10:00 za jioni. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu tuweke kanuni kando ili tuweze kuahirisha kikao chetu kwa sasa na tuweze kuendelea tena na kikao chetu hiki saa 10:00 kamili jioni hii, ili kumuwezesha Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aweze kusoma bajeti ya serikali. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha kikao, kuna tangazo moja. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Mhe. Issa Haji Ussi Gavu, anawatangazia Waheshimiwa Wajumbe wote wanaotoka Mkoa wa Kusini waonane na kuzungumza masuala fulani, hakusema wakutane wapi, lakini nafikiri mwenyewe itakuwa yuko tayari ili kuwaelekeza wapi mkutano huo utafanyika. Hilo ni tangazo na mkutano huo utakuwa mara baada ya kuahirisha kikao hiki.

Pili, jioni tutasikiliza hotuba ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kawaida huwa tunawaalika wageni mbali mbali ili kuja kusikiliza bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo, waweze kujua serikali yao inakusudia kufanya nini kwa mwaka mpya wa fedha kuanzia Julai mwaka huu hadi Juni mwakani. Hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa wageni wetu tumewaomba wafike ukumbini hapa saa 9:30 bara bara wawe wameshakaa pale juu. Basi niwaombe na Waheshimiwa Wajumbe nao tujitahidi kufika mapema, ili tutakapomkaribisha Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aingie na mkoba wake hapa wa bajeti, basi wajumbe wote wawe wameshakaa na wageni pale juu wawe wako tayari kuja kumsikiliza.

Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, haipendezi kuja kuona sasa mmoja mmoja anaingia, au mwengine anaingia kwa kificho hapana, haielekei hivyo. Tufike mapema ili tumkaribishe Mhe. Waziri tena kwa makofi mengi ili kuja kuwasilisha bajeti ya serikali.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe, sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 10:00 jioni leo.

(Saa 4:13 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 10: 00 jioni)

(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyoahirisha kipindi cha asubuhi kwamba leo ni siku ya bajeti na tumewakaribisha wageni mbali mbali. Kwa hivyo, wakati tukimsubiri Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aingie ambapo amejificha pahala na mkoba wake wa bajeti.

Kutokana na hali hiyo, naomba niwataje baadhi ya wageni wetu waliopo ambao tumewaalika. Kwanza kabisa miongoni mwa tuliowaalika yupo Waziri Kiongozi Mstaafu Mhe. Ramadhan Haji Faki namuomba asimame, yule pale. *(Makofi)*

Wakati tunamsubiri Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambapo ofisa wangu sasa anakwenda kumchukua na atakapoingia tutasimamisha na baadaye tutawataja wengine waliohudhuria.

Sasa naomba nimtambue ndugu yetu ambaye ni rafiki yetu Sheikh Abdallah Mohammed Al-Yussuf namuomba asimame, yule pale. Kwa hivyo, kama mnavyojua huyu ndiye aliyetusaidia kwa kushirikiana na serikali kujenga ukumbi wetu huu. *(Makofi)*

Vile vile naomba niwatambue kwa pamoja Makamanda mbali mbali wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama nawaomba kwa pamoja wasimame, wale pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, katika hotuba yetu ya bajeti ya leo tumewakaribisha pia kwanza Katibu Mkuu Kiongozi nimemuona tayari yupo namuomba asimame, yupo pamoja na Makatibu Wakuu mbali mbali wa wizara tofauti pamoja na Manaibu wao nawaomba kwa pamoja wasimame, wale pale. *(Makofi)*

Pia tunao watendaji pamoja na Makatibu Watendaji mbali mbali wa wizara tofauti nawaomba wasimame. *(Makofi)*

Katika Mkutano wetu huu wa leo wa bajeti tuliwakaribisha Mabalozi Wadogo waliopo Zanzibar. *May I now recognise the presence of the Consul Generals based in Zanzibar, could you please rise and salute the members*, nawaomba msimame. *(Makofi)*

Watendaji mbali mbali waliokaribishwa ambao ni pamoja na Kadhi Mkuu, Mufti Mkuu wote nawaomba wasimame.

Waheshimiwa Wajumbe, katika Mkutano huu wa bajeti namuona Mke wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi Mhe. Bi Asha Seif. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo anaingia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wageni wetu mliohudhuria tutawatambua baadaye. Sasa namruhusu Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aanze kusoma Bajeti ya Serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: *Bismillah* Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena umefika wakati wa kutimiza matakwa ya Kifungu cha 105 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kifungu hiki kinamtaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha katika Baraza lako tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata wa fedha kabla ya kumalizika mwaka unaoendelea.

Mhe. Spika, ili kutimiza matakwa hayo ya Katiba, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Baraza lako tukufu likae kama Kamati Maalum ya kujadili na hatimae kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha wa 2012/13.

Mhe. Spika, kama ilivyo desturi, sambamba na hotuba hii, naomba kuwasilisha pia Kitabu cha Kwanza kinachoelezea Mapitio ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2011/12, Kitabu cha Pili kinachotoa Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/13 na Kitabu cha Tatu ambacho ni Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2012/13. Naomba maelezo ya vitabu hivi nayo yawe katika kumbukumbu za Baraza.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kusoma hotuba hii, naomba nitangulize shukurani kwa Muumba wetu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na uzima wa afya na uwezo wa kukutana kwa mara nyengine tena leo hii. Namuomba atujaalie sote hekima, ili tuendeshe kikao chetu kwa maelewano makubwa, utulivu na upendo.

Mhe. Spika, naomba pia nimshukuru mkuu wa nchi yetu, Mhe. Rais, Dr. Ali Mohamed Shein, kwa busara na juhudi kubwa anazozichukua katika kuiongoza vyema Zanzibar kwa lengo la kuiletea maendeleo pamoja na watu wake. Namshukuru pia kwa imani yake kwangu na kuendelea kunipa jukumu hili kubwa la kusimamia masuala ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Napenda kumuahidi kuwa nitatekeleza jukumu hili kwa uwezo wangu wote niliopewa na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako tukufu, naomba kumpongeza Mhe. Rais kwa utaratibu alioanzisha wa kufuatilia kwa ukaribu zaidi matatizo ya wananchi kupitia ziara zake za Mikoa na usimamizi mahiri wa utendaji wa serikali hasa kwa kukutana na wizara na taasisi zake, ili kupata taarifa za mipango na utekelezaji wake pamoja na namna Fedha za Umma zilivyotumiwa. Utaratibu huu umeimarisha zaidi ufanisi katika utendaji wa serikali.

Mhe. Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kuwapongeza Wasaidizi Wakuu wa Mhe. Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais kwa ushauri wao mkubwa kwake ambao umesaidia sana katika kufikia maamuzi yenye hekima na busara. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara, ili waweze kumsaidia vyema Mhe. Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tokea tumalize kikao chetu cha Bajeti cha mwaka jana, kuna matukio mengi ya kuhuzunisha ambayo yametokea nchini kwetu na hapa Barazani. Sote bado tunakumbuka vyema tukio kubwa la msiba lililoikumba nchi yetu, usiku wa tarehe 10 Septemba 2011 lililohusisha kuzama kwa meli ya *MV Spice Islander II*. Mamia ya wananchi wenzetu, wazee, ndugu na watoto wetu, tuliokuwa karibu nao sana walipoteza maisha katika tukio hilo. Tumelia, tumenyamaza, lakini hatujasahau. Kwa mara nyengine tena tunamuomba Mwenyezi Mungu Muweza wa yote azipokee roho za wapendwa wetu na awape malazi mema Peponi, AMIN.

Mhe. Spika, kwa upande wa Baraza lako tukufu, kipindi hichi cha mwaka mmoja tumewapoteza wenzetu wawili, ambao nao wametangulia mbele ya haki, Marehemu Mussa Khamis Silima, aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini na Marehemu Salum Amour Mtondoo aliekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, wote kupitia Chama Cha Mapinduzi, CCM. Tunaungana na familia zao kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu wepesi wa kurudi kwake na malazi mema katika pepo yake tukufu, AMIN.

Mhe. Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali kwa kuchaguliwa kwa kishindo na wananchi wa Jimbo la Uzini kuziba pengo lililoachwa na marehemu Mussa. Sina wasiwasi kuwa wananchi wa Jimbo la Uzini wamepata uwakilishi mwengine mzuri kupitia kwa Mhe. Raza. Nae tunamtakia kila la kheri katika kuwatumikia Wananchi wa jimbo hilo. Aidha, tunasubiri kwa hamu kupata tena uwakilishi wa Jimbo la Bububu wakati utakapokamilika mchakato wa Uchaguzi Mdogo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nianze kwa kuwasilisha Mapitio ya Hali ya Uchumi, Bajeti na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2011/12.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI, BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO 2011/12

Hali ya Uchumi Duniani na Kikanda:

Mhe. Spika, dunia imeendelea kushuhudia kudorora kwa uchumi ukijidhihirisha katika kupungua kwa kasi ya ukuaji wake, kwa ujumla na kwa kila Kanda. Kwa mwaka 2011, uchumi wa dunia umekua kwa wastani wa asilimia 3.9 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5.3 kwa mwaka 2010.

Hali kama hiyo ya kupungua kasi ya ukuaji imejitokeza kwa nchi zilizoendelea, ambapo uchumi wake umekua kwa wastani wa asilimia 1.6 kwa mwaka 2011 ambayo ni nusu tu ya ukuaji wa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2010. Aidha, uchumi wa nchi zinazoendelea umekua kwa wastani wa asilimia 6.2 kwa mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 7.5 iliyoripotiwa mwaka 2010. Mhe. Spika, hali katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, zikiwemo zile za Afrika ya Mashariki haina tofauti sana na taswira hiyo ya dunia. Kasi ya kukua kwa uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara imepungua kutoka wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2010 hadi asilimia 4.9 kwa mwaka 2011.

Upunguaji wa kasi ya ukuaji wa uchumi umejitokeza zaidi katika nchi za Afrika ya Mashariki ambapo ukuaji halisi umepungua kutoka wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2010 hadi asilimia 4.6 mwaka 2011 ambapo kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi ilionekana zaidi katika Sekta ya Umeme, Maji, Ujenzi, Madini, Biashara na Uzalishaji.

Mhe. Spika, kwa ujumla, mwenendo huu usioridhisha wa uchumi duniani unaendelea kusababishwa na matatizo ya kifedha katika nchi za Ulaya, mabadiliko ya tabia nchi, bei kubwa za mafuta na chakula duniani na machafuko ya kisiasa Mashariki ya Kati na baadhi ya maeneo ya Afrika ya Kaskazini kama vile Tunisia, Misri na Libya.

Mwenendo wa Bei Duniani:

Mhe. Spika, mwaka 2011 haukuwa mzuri katika utulivu wa bei. Kasi ya Mfumko wa Bei kwa nchi zilizoendelea na zinazoendelea imepanda kwa bidhaa za chakula na zisizo za chakula. Mfumko wa Bei kwa nchi zilizoendelea umepanda hadi kufikia wastani wa asilimia 2.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.6 kwa mwaka 2010.

Kwa nchi zinazoendelea, Mfumko wa Bei umefikia wastani wa asilimia 7.2 kutoka wastani wa asilimia 6.1 kwa mwaka 2010. Kusini mwa Jangwa la Sahara, Mfumko wa Bei umepanda na kufikia wastani wa asilimia 8.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.4 mwaka 2010.

Kwa upande wa nchi za Afrika ya Mashariki, Mfumko wa Bei umefikia wastani wa asilimia 9.6 mwaka 2011 kutoka wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2010. Kwa ujumla hali hii imetokana na kupanda kwa bei za mafuta na bidhaa za chakula hasa bidhaa za mchele, sukari, mahindi na ngano.

Uchumi wa Zanzibar:

Mhe. Spika, kinyume na mwenendo wa uchumi wa dunia na kikanda, mwaka 2011 Uchumi wa Zanzibar umeonekana kukua vizuri. Pato halisi la Taifa limekuwa kwa asilimia 6.8 na kufikia shilingi 1,198 bilioni (mwaka 2011) kutoka shilingi 946.8 bilioni kwa mwaka 2010. Kasi hiyo ya ukuaji wa asilimia 6.8 ni ya juu

zaidi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Sababu zilizochangia kasi nzuri ya ukuaji wa uchumi wetu ni pamoja na hizi zifuatazo:

i. Kuimarika kwa Sekta ya Huduma kulikochangiwa zaidi na Sekta Ndogo za Biashara, Hoteli na Mikahawa. Kuimarika kwa Sekta Ndogo ya Biashara kumechangiwa zaidi na kuongezeka kwa uzalishaji na bei nzuri ya Karafuu katika soko la dunia. Jumla ya Tani 2,539 za Karafuu zilisafirishwa mwaka 2011 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 19 kutoka Tani 2,132 zilizosafirishwa mwaka 2010. *(Makofi)*

   Usafirishaji huo umepelekea kukua kwa thamani ya usafirishaji nje kwa asilimia 77 kutoka shilingi 11.2 bilioni mwaka 2010 hadi shilingi 50.0 bilioni mwaka 2011. Kwa ujumla, Sekta ya Biashara ilikuwa kwa asilimia 21.5 mwaka 2011 ikiwa ni mara tatu ya ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2010. *(Makofi)*

   Kwa upande wa Sekta Ndogo ya Hoteli na Mikahawa, kumejitokeza ukuaji wa kuridhisha wa asilimia 10.2, ambao ni mara tatu ya ukuaji wa mwaka 2010 wa asilimia 3.0. Ukuaji huu umechangiwa na ongezeko la idadi ya watalii kwa asilimia 31.8 kutoka watalii 132,836 mwaka 2010 hadi kufikia watalii 175,067 mwaka 2011.

ii. Ongezeko la asilimia 30.2 la uwekezaji rasilimali, hususan katika ujenzi wa barabara na madaraja.

iii. Kuimarika kwa Sekta ya Viwanda iliyokua kwa asilimia 5.8 mwaka 2011 ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 1.9 mwaka 2010 kutokana na mwenendo mzuri katika maeneo ya nishati, uchimbaji wa mawe na mchanga pamoja na ujenzi.

Mhe. Spika, ukuaji mzuri wa pato la Taifa uliopindukia kasi ya ongezeko la watu umepelekea kupanda kwa kiwango cha wastani wa pato la mtu binafsi kutoka shilingi 782,000 (USD 560) mwaka 2010 na kufikia shilingi 960,000 (USD 617) mwaka 2011. Kiwango hiki cha pato la mtu binafsi kimevuka lengo lililowekwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi cha shilingi 884,000 ifikapo mwaka 2015. Hali hii inatoa matumaini ya kua Ilani ya CCM inatekelezeka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa upande wa mfumo wa uchumi wetu, bado hakuna mabadiliko makubwa. Sekta ya Huduma inaendelea kuongoza na kwa mwaka 2011 mchango wake umeongezeka kutoka asilimia 42.8 mwaka 2010 hadi asilimia 44 ya Pato la Taifa. Ongezeko hilo limepelekea kupungua kidogo kwa mchango wa Sekta ya Kilimo kutoka asilimia 32.4 mwaka 2010 na kufikia asilimia 32.2 mwaka 2011 na ule wa Sekta ya Viwanda kutoka asilimia 12.6 mwaka 2010 hadi asilimia 12.0 mwaka 2011. Mfumo wetu wa uchumi unaonesha kua bado tuna kazi kubwa ya kushajiisha maendeleo ya Sekta ya Viwanda nchini.

Mfumko wa Bei:

Mhe. Spika, kutokana na mtangamano mkubwa wa uchumi wetu na ule wa dunia hususan katika uagiziaji wa chakula na mafuta na matatizo ya uharamia katika Pembe ya Afrika, athari za mwenendo wa mfumko wa bei duniani na katika Kanda zimeleta msukumo wa bei kwenda juu hapa nchini. Kupanda kwa Mfumko wa Bei katika nchi tunazofanya nazo biashara nako kumechangia kupanda kwa Mfumko wa Bei nchini. Kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2011 imepanda na kufikia asilimia 14.7 ikilinganishwa na asilimia 6.1 kwa mwaka 2010. Kwa ndani ya nchi, kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine kumechangia ongezeko hilo la kasi ya mfumko wa bei.

HALI YA BIASHARA

Biashara na Nchi za Nje:

Mhe. Spika, kutokana na mwenendo mzuri wa Zao la Karafuu kwa mwaka 2011, mwenendo wa sekta ya nje ulikuwa wa kuridhisha ukiambatana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa na huduma. Nakisi katika urari wa biashara ya bidhaa kati ya Zanzibar na nchi za nje imepungua kwa asilimia 8 na kufikia shilingi 102.9 bilioni mwaka 2011 kutoka nakisi ya shilingi 111.2 bilioni mwaka 2010.

Hali hii imetokana na ukuaji mzuri wa usafirishaji wa bidhaa ambapo usafirishaji ulikua kwa asilimia 242.5 kutoka shilingi 17.9 bilioni mwaka 2010 hadi shilingi 61.3 bilioni mwaka 2011. Ukuaji wa usafirishaji ulipindukia ukuaji wa uagiziaji ambao ni asilimia 27.2 kutoka shilingi 129.1 bilioni mwaka 2010 hadi shilingi 164.2 bilioni kwa mwaka 2011.

Uwekezaji Binafsi:

Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi wetu umechangiwa pia na kukua kwa kiwango cha uwekezaji binafsi kilichopanda kwa asilimia 40.2 na kufikia Dola za Marekani (USD) 161.6 milioni mwaka 2011 kutoka USD 115.2 milioni mwaka 2010. Ongezeko hili limetokana na miradi ya biashara ya jumla na reja reja, usafiri, usarifu wa bidhaa, hoteli na mikahawa, maghala na mawasiliano, kilimo uwindaji na misitu, ukodishaji wa nyumba na bidhaa nyenginezo.

Maendeleo ya Kiuchumi:

Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi pekee hautoshi. Kinachotakiwa ni kuwa na ukuaji unaoleta manufaa kwa wananchi walio wengi. Ukuaji wa uchumi utafsirike katika maendeleo ya watu. Kwa upande wetu, juhudi mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa na serikali kupitia utekelezaji wa MKUZA zimesaidia sana katika kuimarika kwa hali na ustawi wa kimaisha kwa wananchi wa Zanzibar. Miongoni mwa mafanikio hayo ni haya yafuatayo:

i. Kupungua kiwango cha uzazi kwa kina mama wenye umri wa miaka 15 - 49 kutoka wastani wa watoto 5.4 mwaka 2004/05 hadi kufikia watoto 5.1 mwaka 2009/10.
ii. Kupungua vifo vya kinamama vinavyotokana na uzazi kutoka vifo 473 mwaka 2006 hadi 279 mwaka 2009 kwa kila mama 100,000.
iii. Kushuka kwa vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja kutoka 61 mwaka 2004/05 hadi vifo 54 mwaka 2009/10 kwa kila vizazi hai 1000.
iv. Kuongezeka kwa wastani wa kuishi wa Mzanzibari wakati wa kuzaliwa hadi kufikia miaka 60 mwaka 2011.
v. Kupungua kiwango cha umasikini wa kipato cha Wazanzibari kwa upande wa huduma za msingi (*Basic Needs Poverty*) kutoka asilimia 49.1 mwaka 2004/05 hadi asilimia 44.4 mwaka 2009/10.
vi. Kuimarika kwa wastani wa uwiano wa walimu kwa wanafunzi na kufikia mwalimu mmoja kwa wanafunzi 27 mwaka 2011 ukilinganishwa na wastani wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 28 mwaka 2010.
vii. Wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilomita tano.
viii. Kushuka kwa kiwango cha watoto chini ya miaka mitano ambao uzito wao haulingani na kimo chao (*Under 5 – Underweight*) kutoka asilimia 39.9 mwaka 1990 hadi asilimia 8.1 mwaka 2010.
ix. Kuongezeka kwa wastani wa watoto waliopata chanjo ya shurua kufikia asilimia 95.8 mwaka 2009 ambapo lengo ni kufikia asilimia 100 mwaka 2015.
x. Kiwango cha watoto chini ya umri wa mwaka mmoja ambao wamepata chanjo zote imefikia asilimia 91.8 kwa mwaka 2009. Ingawa kiwango hichi kilishuka katika mwaka 2010, kupitia juhudi maalum za kuhamasisha jamii kushiriki kwenye chanjo mbali mbali kwa watoto kama shurua, polio na utoaji wa matone ya vitamini A hali iliimarika.

Taarifa za mwaka 2012 zinaonesha kwamba asilimia 92 ya watoto chini ya miaka mitano wamepatiwa chanjo ya polio, asilimia 95 wamepatiwa matone ya vitamini A na asilimia 94.2 wamepatiwa dawa za minyoo.

SEKTA YA FEDHA

Huduma za Benki:

Mhe. Spika, matokeo mengine mazuri yaliyojitokeza mwaka 2011 ni kuimarika kwa huduma za fedha nchini. Wakati Amana za benki ziliongezeka kwa aslimia 12.9 kutoka shilingi 311.88 bilioni Machi 2011 na kufikia shilingi 352.07 bilioni Machi 2012, mikopo kwa Sekta Binafsi imekuwa kwa asilimia 46.4 kutoka shilingi 100.36 bilioni hadi shilingi 146.89 bilioni katika kipindi hicho. Uwiano wa mikopo na amana ulifikia asilimia 41.7 mwezi wa Machi 2012, kutoka asilimia 32.2 mwezi Machi 2011.

Mhe. Spika, jambo la kufurahisha ni kuona kuwa wananchi wamehamasika katika kuchukua mikopo. Hadi kufikia mwezi Machi 2012 mikopo iliyotolewa kwa matumizi ya watu binafsi (*personal loans*) imefikia shilingi 53.40 bilioni ambayo ni zaidi ya thuluthi moja ya mikopo yote (36.4%).

Sehemu nyengine ya mikopo hii imeelekezwa zaidi katika Sekta za Kiuchumi, ambapo Sekta ya Biashara imeongoza katika kundi hili kwa kukopa shilingi 28.18 bilioni sawa na asilimia 19.2 ya mikopo yote na Sekta ya Utalii ilikopa jumla ya shilingi 22.38 bilioni, sawa na asilimia 15.2.

Aidha mikopo katika Sekta ya Ujenzi ilifikia shilingi 6.51 bilioni, sawa na asilimia 4.4 na Sekta ya Usafiri ilifikia shilingi 3.06 bilioni, sawa na asilimia 2.1. Hali hii inaashiria kuongezeka kwa matumizi ya benki sio tu kwa kuhifadhi fedha za wateja na kujiwekea akiba, lakini pia katika kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali 2011/12

Mhe. Spika, serikali ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya TZS 613.08 bilioni katika mwaka wa fedha 2011/12 unaoendelea. Kati ya mapato hayo, TZS 241.84 bilioni ikiwemo mapato ya kodi na yasiyo ya kodi pamoja na mikopo ya ndani na kiasi kilichobakia cha TZS TZS 371.24 bilioni zilitarajiwa kutokana na Washirika wa Maendeleo. Kwa upande wa Matumizi, TZS 234.18 bilioni ziliidhinishwa kutumika kwa kazi za kawaida na TZS 378.9 bilioni kwa kazi za maendeleo. Muhtasari wa mwenendo wa mapato na matumizi kwa kipindi cha miezi tisa hadi Machi 2012 ni kama hivi ifuatavyo.

Mapato ya Ndani

Mhe. Spika, kati ya mapato ya ndani yaliyokadiriwa ya TZS 221.2 bilioni sawa na asilimia 18.5 ya pato la taifa, TZS 210.2 bilioni zilitarajiwa zitokane na vianzio vya kodi na TZS 11.02 bilioni ni kutokana na vyanzo visivyokuwa vya kodi. Kati ya TZS 210.2 bilioni zilizotokana na kodi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ilikadiriwa kukusanya TZS 100.6 bilioni zikiwemo TZS 18 bilioni kutokana na Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaofanya kazi Zanzibar. Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) ilitarajiwa kukusanya kiasi kilichobakia cha TZS 109.6 bilioni. ZRB ilitarajiwa pia kukusanya TZS 11.02 bilioni za mapato yasiyo ya kodi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2011 hadi Machi mwaka 2012), Serikali ilikadiria kukusanya mapato ya ndani ya TZS 170.3 bilioni. Makusanyo halisi yalifikia TZS 169.6 bilioni sawa na asilimia 99.6 ya makadirio ya kipindi hicho. Ikilinganishwa na mwaka uliopita (2010/2011) katika kipindi kama hicho, kunajitokeza ukuaji wa mapato kwa asilimia 27.6. Kati ya makusanyo hayo, mapato kutokana na kodi yalifikia TZS 152.1 bilioni ambazo sawa na asilimia 94.1 ya makadirio. Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 17.5 bilioni sawa na asilimia 198.9 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya mapato yasiokuwa ya kodi, TZS 7.8 bilioni ni gawio la faida kutoka Benki Kuu na TZS 9.7 bilioni ni mapato ya kutoka Mawizarani.

Mhe. Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato kitaasisi, katika kipindi cha miezi tisa (Julai – Machi 2011/12), TRA imekusanya jumla ya TZS 67.1 bilioni sawa na asilimia 88.6 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 75.7 bilioni. Kutofikiwa kwa lengo hilo kumetokana zaidi na kutolipwa kwa TZS 15.5 bilioni za kodi ya mapato kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar. Ikilinganishwa na mwaka uliopita (2010/2011) katika kipindi kama hicho, kunajitokeza ukuaji wa mapato wa asilimia 20.4. Aidha Bodi ya Mapato Zanzibar ilikusanya jumla ya TZS 94.7 bilioni sawa na asilimia 100.7 ya makadirio kutokana na mapato ya kodi na yasiyokuwa ya kodi sawa na ukuaji wa asilimia 22.7 ikilinganishwa na mwaka uliopita katika kipindi kama hicho. Kati ya TZS 94.7 bilioni, mapato ya kodi yalifikia TZS 84.9 bilioni sawa na asilimia 99.0 ya makadirio.

Mhe. Spika, Kodi ya Ongezeko la Thamani, Ushuru wa bidhaa za Petroli na Ushuru wa bidhaa zimechangia TZS 64.8 bilioni sawa na asilimia 38.2. Mchango wa Ushuru wa Forodha ni TZS 43.0 bilioni sawa na asilimia 25.4, Kodi ya Mapato kutokana na ajira TZS 12.9 bilioni sawa na asilimia 7.6, wakati mchango wa Kodi Nyenginezo ulifikia TZS 41.0 bilioni sawa na asilimia 24.1 ya mapato yote ya ndani.

MATARAJIO YA MAPATO HADI JUNI 2011/12

Mhe. Spika, kutokana na utendaji wa miezi tisa na matarajio ya robo mwaka ya Aprili – Juni, inatarajiwa kwamba mapato ya ndani kwa mwaka mzima yatafikia TZS 217.1 bilioni sawa asilimia 98.1 ya makadirio. Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 88.9 bilioni sawa na asilimia 88.4 ya makadirio, wakati Bodi ya Mapato Zanzibar inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 120.4 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 100.4 ya makadirio kutokana na mapato ya kodi na yasio ya kodi.

Mhe. Spika**,** kati ya TZS 120.4 bilioni, mapato ya kodi yatafikia TZS 108.3 bilioni sawa na asilimia 98.7 ya makadirio wakati mapato yasiyokuwa ya kodi kutoka katika Wizara za Serikali yatafikia TZS 12.1 bilioni sawa na asilimia 118 ya makadirio.

Mapato ya Nje

Mhe. Spika, katika mwaka wa 2011/12, Serikali ilipanga kupokea jumla ya TZS 371.24 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zikiwemo TZS 30.28 bilioni za Misaada ya Kibajeti (GBS) na TZS 340.96 bilioni zikiwa mikopo na ruzuku kwa Programu na Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, ruzuku ni TZS 124.96 bilioni na mikopo TZS 216.0 bilioni.

Mhe. Spika, hadi Machi 2012, jumla ya TZS 199.0 bilioni sawa na asilimia 53.6 ya matarajio ya mwaka zilipatikana zikiwemo TZS 24.1 bilioni za Misaada ya Kibajeti sawa na asilimia 79.7. Aidha jumla ya TZS 174.9 bilioni zilipatikana kupitia programu na miradi mbali mbali ikiwa sawa na asilimia 51.3 ya matarajio.

Mhe. Spika, matarajio ni kupatikana TZS 202.1 bilioni ambazo zitakuwa sawa na asilimia 59.3 ya matarajio ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa mwaka 2011/12. Mapato kutokana na misaada ya kibajeti yanatarajiwa kufikia TZS 30.3 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka.

DENI LA TAIFA

Mhe. Spika, hadi mwezi wa Machi, 2012 Deni la Taifa limefikia TZS 209.9 bilioni sawa na asilimia 15 ya Pato la Taifa. Kati ya kima hicho cha Deni, Deni la Ndani ni TZS 49.4 bilioni linalohusisha dhamana za Hazina na Hati Fungani za TZS 30.4 bilioni zinazotarajiwa kuwa tayari kulipwa kati ya Agosti 2012 na Julai 2016. Deni la Nje ni TZS 160.5 bilioni (USD 102.0 milioni). Hadi kufikia Machi 2012 deni la Kiinua Mgongo lilifikia jumla ya TZS 2.4 bilioni ambapo jumla ya TZS 4.04 bilioni zililipwa kwa wastaafu 604 katika kipindi cha Mapitio. Tunatarajia kumaliza mwaka wa 2011/12 na deni la Kiinua Mgongo kwa ujumla litafikia TZS 4.5 bilioni kwa wafanyakazi watakaostaafu mwezi wa Aprili hadi Juni 2012.

UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO

Mhe. Spika, katika Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana nilieleza dhamira ya Serikali ya kutopandisha viwango vya kodi na badala yake kuimarisha usimamizi wa kodi zilizopo. Moja ya eneo lililokuwa likilalamikiwa sana katika kuikosesha Serikali mapato ni uingizaji wa mafuta ya petroli kwa njia ya magendo. Hatua maalum ilibidi kuchukuliwa ili kukabiliana na uhalifu huo.

Mhe. Spika, katika kipindi hichi, Serikali imepiga marufuku utaratibu uliokuwa ukitumika kwa kuingiza mafuta kwa kuuziana bahari kuu na kuhamisha meli moja kwenda nyengine. Utaratibu huu ulibainika kuwa ndio chanzo kikuu cha magendo. Sambamba na hatua hiyo, Serikali kupitia ZRB na Polisi na Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) ilifanya zoezi maalum la kupambana na magendo hayo. Matokeo ya zoezi hilo ni kukamatwa jumla ya lita 165,523 ya mafuta ya nishati yaliyokuwa yakiingizwa nchini kwa magendo.

Mhe. Spika, hatua nyengine za kiutawala zililenga katika kuongeza ujuzi kwa wasimamizi wa kodi wa TRA na ZRB, kusajiliwa katika mtandao wa kodi kwa wafanyabiashara wapya 290 Pemba na Unguja na kufanya ukaguzi wa pamoja baina ya TRA na ZRB kwa baadhi ya walipa kodi.

Mhe. Spika, hatua moja ambayo haikutekelezwa katika kipindi hiki ni kukusanywa kwa kodi ya mapato ya wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano waliopo Zanzibar. Hatua hii ilitarajiwa kuingiza jumla ya TZS 18 bilioni. Utekelezaji ulitegemea kutekelezwa na SMT kwa makubaliano hayo kwa serikali mbili. Kwa bahati mbaya utekelezaji haukuanza katika mwaka wa 2011/12 na hivyo kuathiri kiwango cha utendaji cha TRA na Bajeti ya SMZ kwa ujumla. Matarajio yetu ni kuwa utekelezaji huo sasa utaanza katika mwaka ujao wa fedha baada ya marekebisho ya Sheria yanayohitajika.

MATUMIZI YA SERIKALI MWAKA 2011/12

Makadirio ya matumizi ya Serikali

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2011/12 jumla ya TZS 613.1 bilioni zimekadiriwa kutumika. Katika kipindi cha tathmini, matumizi halisi yamefikia TZS 377.0 bilioni sawa na asilimia 117.3 ya makadirio ya miezi tisa ya TZS 321.5 bilioni. Kati ya matumizi hayo TZS 174.9 bilioni ni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 99.7 ya makadirio ya miezi tisa ya TZS 175.4 bilioni. Kwa upande wa kazi za maendeleo matumizi yalifikia TZS 202.1 bilioni sawa na asilimia 138.3 ya TZS 146.1 bilioni ya makadirio ya miezi tisa. Kati ya fedha hizo TZS 27.2 bilioni ni fedha za ndani na TZS 174.9 bilioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya matumizi ya TZS 469.4 bilioni yanayotarajiwa hadi Juni 2012, TZS 228.6 bilioni sawa na asilimia 48.7 ni matumizi ya Kazi za Kawaida na TZS 240.8 bilioni sawa na asilimia 51.3 ni kwa kazi za maendeleo.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2011-MACHI 2012

Mhe. Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2011/12, Serikali ilikamilisha mapitio na marekebisho ya Dira ya Maendeleo ya 2020 ya Zanzibar, Utayarishaji wa Mpango wa miaka mitano wa utekelezaji wa MKUZA II, Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji wa MKUZA II na Tathmini ya Hali ya Mahitaji ya Wataalamu Nchini. Ili mipango hii ieleweke vizuri na kufanyiwa kazi na wananchi, hatua maalum za uelimishaji na uenezi zitachukuliwa.

Mhe. Spika, lengo kuu la Dira ya 2020 ni kuondoa umasikini uliokithiri, kuwa na Maendeleo endelevu pamoja na uchumi wa kisasa unaohimili ushindani. Kwa kuwa nusu ya kipindi cha utekelezaji wa Dira kimemalizika, Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Dira 2020 na hatimae kufanya marekebisho ya muelekeo kwa miaka 10 ijayo kutokana na mambo yaliyojitokeza yakiwemo haya yafuatayo:

i. Kwamba uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika lakini ukuaji wake haukufikia kiwango kilichotarajiwa.

ii. Kumepatikana mafanikio mazuri katika kupunguza umaskini usio wa kipato kutokana na kupiga hatua katika huduma za jamii hususan elimu na afya. Hata hivyo, ukuaji wa uchumi haujapunguza sana umaskini wa kipato.

iii. Kuna Maendeleo makubwa yaliofikiwa katika kuimarisha Utawala Bora hususan katika uhuru wa kujieleza, uwajibikaji na utulivu wa kisiasa.

Mhe. Spika, matokeo haya ya tathmini ya utekelezaji wa Dira yetu ya 2020 yanabainisha kuwa pamoja na mafanikio tuliyoyapata katika nusu ya kwanza ya utekelezaji, bado tuna kazi kubwa ya kutekeleza katika nusu iliyobakia. Kazi hii inahusisha kujenga uchumi imara na wenye ushindani, kukuza hali za maisha ya jamii yetu na kuimarisha utawala bora. Ili kufanikisha matarajio hayo, Taarifa ya Mapitio imependekeza mambo ya kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano (2010-2015) yakiwemo haya yafuatayo:

i. Kuwekeza katika mageuzi ya kitaasisi hasa katika utumishi wa umma;

ii. Uwekezaji stadi wa rasilimali watu;

iii. Kuweka vipaumbele vya msingi katika uwekezaji wa miundombinu ya usafirishaji, maji, umeme na mawasiliano;

iv. Kuimarisha taasisi, sera na sheria ili kuhakikisha kuwepo kwa uwiano baina ya shughuli za watu na miundombinu ya mtandao; na

v. Kuimarisha Mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya MKUZA.

Mhe. Spika, kwa bahati njema, Mapendekezo haya yanashabihiana na mambo yaliyomo katika MKUZA II na hivyo tutakapoutekeleza vyema tutakuwa pia tumetekeleza Mapendekezo ya Mapitio ya Dira ya 2020. Ili kutekeleza MKUZA II, Serikali imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa miaka mitano na kubainisha Mpango wa

Uwekezaji Rasilimali wenye jumla ya Programu na Miradi 165. Jumla ya Dola za Kimarekani 2.7 bilioni zinahitajika kuutekeleza. Serikali itashirikiana na Sekta binafsi kuhakikisha kuwa nayo inashiriki kikamilifu katika uwekezaji huo.

Mhe. Spika, ili kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa MKUZA II pamoja na kuwezesha kuchukuliwa hatua za marekebisho kwa wakati na Serikali na watekelezaji wengine, umeandaliwa Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji na Tathmini. Dhamira kuu ya Mpango huo ni kupata taarifa sahihi za Mpango wa utekelezaji na matumizi ya rasilimali, hali ambayo itasaidia kuchukuliwa kwa wakati hatua za kurekebisha kasoro zinazojitokeza.

Mhe. Spika, tathmini ya hali ya mahitaji ya wataalamu nchini imeonesha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya wafanyakazi katika sekta rasmi ni wenye elimu chini ya kidato cha sita. Maeneo yaliyobainika kuhitaji kipaumbele zaidi katika Mpango wa Mafunzo wa Miaka Mitano (2012-2016) ni pamoja na Udaktari wa fani mbali mbali pamoja na watumiaji wa vifaa vya afya *(medical imaging)*, Wafamasia, Wachumi, Uvuvi, Kilimo, Utawala wa Biashara, Ununuzi *(Procurement)*, Mifugo *(Veterinary)* Utafiti, Usimamizi wa Hoteli na Utalii, Utaalamu wa Madini ikiwa ni pamoja na mafuta *(petroleum), (giologia)*, Mipango, Usimamizi Rasilimali Watu, Usimamizi wa Fedha, Teknologia ya Habari na Mawasiliano, Ualimu wa Sayansi na Hesabati, Uhandisi, Usanifu majengo (*Architecture*), Takwimu na Utaalamu wa Mazingira. Fani hizo ndizo zitakazopewa kipaumbele katika utoaji wa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema, jumla ya TZS 378.9 bilioni ziliidhinishwa kugharamia utekelezaji wa Programu 27 na Miradi 77 ya Maendeleo kwa mwaka 2011/12. Kati ya fedha hizo zilizopangwa, TZS 37.9 bilioni sawa na asilimia 10.1 zilitarajiwa kutolewa na Serikali na TZS 340.9 bilioni sawa na asilimia 89.9 zilitarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2011-Machi 2012 jumla ya TZS 202.1 bilioni sawa na asilimia 53.3 zilitolewa kugharamia utekelezaji wa Programu/Miradi. Kati ya fedha hizo, (TZS 202.1 bilioni), TZS 27.2 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 13.5 zimetolewa na Serikali na TZS 174.9 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 86.5 ni mchango wa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu MKUZA umepangwa ki-Klasta. Klasta ya kwanza ya Ukuzaji Uchumi na Upunguzaji Umasikini wa Kipato ilitarajiwa kutekeleza jumla ya Programu 17 na Miradi 17 na kutengewa jumla ya TZS 183.2 bilioni sawa na asilimia 48.4 ya bajeti ya kazi za Maendeleo. Serikali ilitenga jumla ya TZS 15.8 bilioni sawa na asilimia 8.6 na wakati Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia jumla ya TZS 167.5 bilioni sawa na asilimia 91.4 ya bajeti ya Klasta hii.

Hadi kufikia Machi 2012, Klasta ya kwanza imepatiwa jumla ya TZS 113.2 bilioni sawa na asilimia 62 ya bajeti ya mwaka ya Klasta hiyo na sawa na asilimia 58 ya bajeti ya mwaka ya kazi za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali imetoa TZS 11.6 bilioni sawa na asilimia 74 ya makadirio yake kwa Klasta hii na Washirika wa Maendeleo wamechangia kiasi cha TZS 101.6 bilioni sawa na asilimia 61.

Mhe. Spika, Klasta ya Huduma na Ustawi wa Jamii ilipangiwa kutekeleza jumla ya Programu 6 na Miradi 33 ya Maendeleo kwa gharama ya TZS 151.5 bilioni, sawa na asilimia 39.9 ya bajeti ya Maendeleo. Serikali ilitenga jumla ya TZS 12.9 bilioni sawa na asilimia 8.5 ya bajeti ya Klasta na Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia jumla ya TZS 138.6 bilioni sawa na asilimia 91.5.

Mhe. Spika, hadi kufikia Machi 2012, Klasta hii imepatiwa kiasi ya TZS 46.5 bilioni sawa na asilimia 27.5 ya fedha zilizotolewa kwa utekelezaji wa Programu/Miradi ya Maendeleo, ambayo ni sawa na asilimia 31 ya makadirio ya matumizi ya Klasta hii. Serikali imetoa TZS 10.4 bilioni sawa na asilimia 81 ya makadirio yake ya mwaka na Washirika wa Maendeleo wamechangia TZS 36.1 bilioni sawa na asilimia 26.

Mhe. Spika, Klasta ya tatu ni ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa. Kwa mwaka 2011/12 Klasta hii ina Programu nne na Miradi 27 ya Maendeleo iliyotarajiwa kutekelezwa iliyopangiwa kutumia TZS 44.2 bilioni sawa na asilimia 11.7 ya bajeti ya Maendeleo. Serikali ilitenga jumla ya TZS 9.3 bilioni sawa na asilimia 21 na Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kuchangia jumla ya TZS 34.9 bilioni sawa na asilimia 78.9 ya bajeti ya Klasta ya tatu. .

1. Hadi kufikia Machi 2012, Klasta imepokea jumla ya TZS 36.5 bilioni sawa na asilimia 83 ya makadirio yake ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Serikali imetoa TZS 5.1 bilioni sawa na asilimia 55 ya makadirio

yake na Washirika wa Maendeleo wamechangia TZS 31.4 bilioni sawa na asilimia 90 ya makadirio ya Klasta ya tatu.

UTEKELEZAJI WA MAENEO YALIYOPEWA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2011/12

Kuimarisha huduma za afya

Mhe. Spika, serikali iliendelea na zoezi la mfumo wa kupeleka dawa kulingana na mahitaji halisi ya kituo, ambapo vituo 19 vimo katika Mpango huo wa majaribio. Aidha, hospitali ya Mnazi mmoja inaendelea kushirikiana na madaktari wa nje mbali mbali kuendesha kambi za operesheni. Katika kipindi cha miezi tisa cha Julai 2011 hadi Machi 2012, jumla ya wagonjwa 822 wamefanyiwa uchunguzi, kati yao wagonjwa 199 walifanyiwa upasuaji na Serikali kuokoa jumla ya Dola za Kimarekani 1.6 milioni kama wangesafirishwa nje ya nchi. Mashine mbili za kuhifadhia dawa za chanjo kwa ajili ya chanjo mpya ya kuzuia maradhi ya kuharisha pamoja na vifaa mbali mbali vya chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) vimenunuliwa. Ujenzi wa bohari kuu ya madawa unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Juni 2012.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio niliyoyaeleza awali, moja ya changamoto kubwa inayoikabili sekta ya afya ni idadi kubwa ya vifo vya mama na watoto. Serikali imeamua kuchukua hatua maalum za kukabiliana na hali hii. Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na malalamiko kutokana na hatua ya serikali kutoza fedha kutoka kwa akina mama ili kuchangia huduma za kujifungua. Hali yetu ya fedha sasa imeimarika kiasi, na hivyo serikali inaweza kubeba jukumu hili bila ya kuathiri ubora wa huduma. Kama mtakavyokumbuka, wakati akiwa katika ziara Mkoa wa Kusini Unguja mnamo tarehe 9 Mei mwaka huu, Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein aliagiza kusitishwa kwa tozo hilo kwa akina mama.

Mhe. Spika, nina furaha kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa utekelezaji wa agizo hilo muhimu lililotolewa na Mhe. Rais utaanza rasmi tarehe 1 Julai, 2012 na hivyo akina mama wanaojifungua katika hospitali za serikali hawatachangia tena, na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itagharamia gharama za kujifungua kwa akina mama hao.

Kuimarisha ubora wa elimu

Mhe. Spika, jumla ya madarasa 80 kati ya 200 ya skuli za msingi yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi yamekamilika na kuanza kutumika Unguja na Pemba. Aidha, jumla ya madeski 500 kwa skuli za msingi yamechongwa na kusambazwa katika skuli za Unguja na Pemba. Vile vile, skuli mpya tatu za sekondari zimekamilika na nyengine tisa ziko katika hatua za kukamilishwa. Walimu 186 wameajiriwa katika skuli mbali mbali Unguja na Pemba.

Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama

Mhe. Spika, uchimbaji wa visima vitatu katika maeneo ya Chumbuni na kisima kimoja katika Kituo Kikuu Saateni kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa huduma ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi umekamilika. Aidha, kazi za ulazaji wa mabomba mapya imefanyika kwa maeneo ya Kinuni, Kijichi, Magomeni, Mpendae, Chuini na Kihinani. Kwa upande wa Pemba uchimbaji wa visima, Ujenzi wa vituo, Ujenzi wa *'wellhead'* pamoja na upelekaji wa umeme umekamilika kwa maeneo ya Chokocho, Michenzani, Junguni na Konde.

Kuimarisha sekta ya kilimo

Mhe. Spika, kwa upande wa miundombinu ya umwagiliaji, msingi mkubwa wa mita 670 na msingi wa ndani wa udongo wa mita 150 katika bonde la Bumbwisudi; mtaro wa saruji wa mita 200 katika bonde la Makombeni Pemba na mita 525 Kianga imejengwa. Ujenzi wa barabara ya kifusi mita 100 umefanyika Bumbwisudi; Pia tani 1090 za mbolea aina ya TSP 545 na Urea zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima.

Mhe. Spika, serikali imeendeleza juhudi za kuimarisha kilimo cha mpunga wa NERICA baada ya majaribio ya mbegu hii kuonesha mafanikio. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012 jumla ya tani 21 za mbegu zilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima na wazalishaji mbegu. Aidha mashamba ya mfano wa uzalishaji yamefanywa kwa shehia 230 Unguja na Pemba ili wananchi wapate kujifunza njia bora za ukulima na upandaji wa NERICA. Sambamba na hayo, mabwana shamba 183 na maafisa wilaya 18 pia wamepewa mafunzo hayo.

Kuanza kuweka Mazingira Bora ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi:

Mhe. Spika, mchakato wa kutayarisha Sera ya Uwezeshaji umeanza katika hatua za awali. Mafunzo ya mbinu za uandishi na utunzaji wa vitabu vya hesabu yametolewa kwa Wajasiriamali pamoja na uendelezaji wa Soko la Jumapili kwa Wajasiriamali katika eneo la Michenzani. Aidha, katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2011-Machi 2012), jumla ya shilingi 62.9 milioni zimetolewa kupitia Mfuko wa JK/AK na shilingi 97.5 milioni kutoka Mfuko wa Kujitegemea. *(Makofi)*

Kuendeleza Tafiti mbali mbali:

Mhe. Spika, jaribio la mbegu za aina tatu za mpunga zenye kustahamili maradhi ya ugonjwa wa manjano ya majani ya mpunga limefanyika pamoja na kufanya uchunguzi wa aina 15 za mbegu za mpunga; Tafiti za mbegu mpya aina 70 za mpunga zinaendelea. Uchunguzi wa udongo katika mabonde ya Mziwanda Pemba umefanyika na kuendeleza utafiti na udhibiti wa wadudu aina ya chonga.

Mhe. Spika, kwa upande wa sekta ya afya utafiti wa maradhi yasiyoambukiza (NCD) ulifanyika mwaka 2011 na kuonekana kuwa maradhi ya sukari, sindikizo la damu yameongezeka kwa kasi katika visiwa vyetu kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha. Aidha, katika Sekta ya Nishati, Serikali kwa msaada wa Jumuiya ya Ulaya, imefanya tathmini ya fursa ya aina ya nishati anuwai nchini kwa kuzingatia nishati kutokana na jua, upepo na taka.

Matokeo ya awali yameonesha kuwa kisiwa cha Unguja kina fursa ya kuzalisha umeme kwa njia ya upepo, ili kusaidiana na ule wa nguvu za maji unaonunuliwa kutoka *TANESCO* Tanzania Bara. Serikali inaendelea kufanya tafiti nyengine katika maeneo mbali mbali.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI 2012/13

Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia:

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Shirika la Fedha Duniani (*IMF*), hali ya kupungua kwa kasi ya ukuaji wa inatarajiwa kuendelea katika mwaka 2012. Uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.5 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.9 kwa mwaka 2011.

Uchumi wa nchi zilizoendelea nao pia unatarajiwa kukua kwa asilimia 1.4 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.6 kwa mwaka 2011. Hii ni kutokana na kutotengamaa kwa uchumi katika nchi nyingi zilizoendelea tokea kutokea Mtikisiko wa Uchumi wa dunia mwaka 2008 na tatizo la madeni lililozikumba nchi za Ulaya.

Mhe. Spika, hali ya kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa pia kuonekana katika nchi zinazoendelea, ambapo uchumi wake utakuwa kwa wastani wa asilimia 5.7 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.2 kwa mwaka 2011.

Kwa baadhi ya nchi katika Bara la Asia, hali hii itachangiwa zaidi na kushuka kwa usafirishaji wa bidhaa kwenda nchi zilizoendelea, wakati kwa nchi zilizo katika Bara la Afrika na baadhi ya nchi zilizo Marekani ya Kusini, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kupungua kutokana na kushuka kwa bei za bidhaa zinazozalishwa nchini humo katika soko la dunia.

Mhe. Spika, kwa ujumla mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kuwa tofauti na mwenendo wa dunia na kanda nyengine. Uchumi wa nchi hizo unatarajiwa kukuwa kwa kasi zaidi kufikia ukuaji wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 5.1 kwa 2011. Kasi hii inachangiwa na kuvumbuliwa kwa visima vipya vya mafuta na upatikanaji wa madini kwa nchi kama vile Uganda, Angola na Kenya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusiana na mwenendo wa bei, taswira inayojitokeza ni ya kutia moyo. Mfumko wa bei kwa nchi zilizoendelea unatarajiwa kushuka hadi kufikia asilimia 1.9 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 2.7 kwa mwaka 2011.

Aidha, mfumko wa bei kwa nchi zinazoendelea unatarajia kushuka hadi kufikia asilimia 6.2 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2011. Kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za chakula

duniani pamoja na matarajio ya kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia kutasaidia kupunguza kasi ya mfumko wa bei duniani.

Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar:

Mhe. Spika, Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2012 unatarajiwa kuimarika zaidi. Utekelezaji wa malengo ya uchumi unatarajiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, MKUZA II, Malengo ya Milenia pamoja na Mageuzi ya Msingi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012, Uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.5 kutoka ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2011. Matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2012 yanatokana na mambo yafuatayo:

i. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya biashara hasa zao la karafuu.
ii. Kuongezeka kwa uwekezaji binafsi ikiwa pamoja na miradi ya uvuvi wa bahari kuu, kilimo na miradi ya utalii.
iii. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii nchini kutokana na hatua mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa na taasisi mbali mbali za kuutangaza utalii wa Zanzibar. Lengo ni utalii kwa wote, ambao utatuwezesha kila mmoja wetu kuweza kushiriki katika kuutangaza utalii wetu. *(Makofi)*
iv. Kukamilika kwa uwekaji wa waya wa umeme wa chini ya bahari kutoka Rasi Kiromoni ya Tanzania Bara hadi Rasi ya Fumba. Ukamilikaji wa zoezi hilo litawezesha upatinakaji wa umeme wa uhakika katika Kisiwa cha Unguja, ambapo utasaidia kushajihisha maendeleo ya kiuchumi.
v. Utekelezaji wa *Program* ya Mageuzi ya Kilimo Zanzibar, ambayo itashajihisha uzalishaji na kuongeza tija na kuhakikisha uhakika wa chakula.
vi. Kuimarika zaidi kwa mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Binafsi (*Public Private Partnership*), ambapo Sekta Binafsi inatarajiwa kuwa ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi.

Mhe. Spika, sambamba na matarajio ya kushuka Mfumko wa Bei duniani, kasi ya Mfumko wa Bei nchini nayo unatarajiwa kushuka hadi kufikia asilimia 8.7 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 14.7 mwaka 2011. Mbali na mwenendo wa bei duniani, kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa mazao ya chakula na biashara, kuimarika kwa Sekta ya Uvuvi na kuendelea kuimarika kwa thamani ya sarafu ya Tanzania nako kunatarajiwa kushusha msukumo wa Mfumko wa Bei.

MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO – 2012/13:

Mhe. Spika, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/13 utategemea zaidi utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 iliyorekebishwa, MKUZA II, pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha CCM ya mwaka 2010. *(Makofi)*

MAENEO YA KIPAUMBELE

Kuimarisha Huduma ya Afya:

Mhe. Spika, umuhimu wa huduma bora za afya sote tunaufahamu na hauhitaji kusisitizwa zaidi. Serikali ya Awamu ya saba imeweka mkazo maalumu katika kuimarisha huduma hizi hususan katika kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na nyenzo mbali mbali za utibabu, kuvipandisha hadhi vituo vya afya na hospitali hatua kwa hatua na kuimarisha huduma za uzazi kwa mama na mtoto.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imedhamiria kuhakikisha kuwa ndani ya miaka mitatu ijayo, inabeba jukumu lote la upatikanaji wa dawa na nyenzo za utibabu na kuacha kutegemea wafadhili katika eneo hilo muhimu. *(Makofi)*

Kuanzia mwaka ujao wa fedha, bajeti ya ununuzi wa dawa itakuwa inaongezwa kila mwaka hadi lengo hilo lifikiwe. Sambamba na ununuzi huo wa dawa na nyenzo za utibabu, serikali pia itakuwa inatenga fedha kwa ununuzi wa vifaa vyengine vya afya vinavyohitajika. *(Makofi)*

Kuimarisha Ajira kwa Vijana:

Mhe. Spika, karibu theluthi mbili (asilimia 63.1) ya watu katika jamii yetu ni ama watoto au vijana wasiopindukia umri wa miaka 24. Kwa upande mwengine, idadi kubwa ya vijana wetu wanamaliza skuli na

kuingia katika soko la ajira kila mwaka. Takwimu zinaonesha kuwa kati ya vijana watano (asilimia 17 ya vijana) wenye umri wa kati ya miaka kumi na tano hadi ishirini na nne (24) mmoja hana ajira. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hali hii inamaanisha kuwa tatizo la ajira kwa vijana ni kubwa na linahitaji hatua makhsusi. Kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali imeandaa Programu maalumu ya kuwawezesha vijana katika shughuli za kiuchumi ikiwemo uvuvi, kilimo, kazi za usafi wa mji, ujasiri amali na utalii. Programu hii ni hatua moja muhimu ya kukabiliana na tatizo la ajira.

Hata hivyo, ili mafanikio kamili yaweze kupatikana, tunahitaji pia kuwafunza vijana wetu kubadilika katika mkabala wetu na kazi na kupunguza kuchagua sana aina ya kazi.

Kuimarisha Ustawi wa Wazee:

Mhe. Spika, miongoni mwa malengo ya Mapinduzi Matukufu ya 1964 ni kuimarisha ustawi wa wananchi wote, ikiwemo wa makundi yenye mahitaji maalum kama vile Wazee. Katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana nilitangaza kuongezwa kwa posho la Wazee wanaotunzwa na serikali kutoka shilingi elfu kumi na tano hadi elfu arobaini na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuimarisha hali za wazee kadiri hali ya uchumi inavoruhusu.

Hata hivyo, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar alipowatembelea wazee aliifafanua dhamira ya Serikali katika kuwahudumia wazee hao.

Mhe. Spika, ahadi ile ya serikali itaendelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/13, ili kudumisha huduma kwa wazee wanaohudumiwa na serikali, kuanzia mwaka ujao wa fedha. Serikali itawapatia wazee wanaoishi katika Kituo cha Sebleni huduma kamili ya chakula, posho na matibabu. Wazee pia watapatiwa vitambulisho vitakavyowawezesha kupata huduma mbali mbali kwa utaratibu maalum. Huduma kama hizi kwa wazee wanaoishi Welezo zinakwenda vizuri. *(Makofi)*

Kuimarisha Elimu:

Mhe. Spika, hakuna nchi inayoweza kuendelea bila ya kuwa na jamii iliyoelimika vya kutosha. Kwa kutambua ukweli huu, serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali kuimarisha upatikanaji, usawa na ubora wa elimu nchini. Elimu ya lazima itaimarishwa kwa kuendeleza ujenzi wa skuli za ghorofa za Kiembe Samaki, Mpendae, Kwamtipura, Kibuteni na Mkanyageni pamoja na ununuzi wa madawati na vifaa vya kusomea na kufundishia. *(Makofi)*

Aidha, Mfuko wa Elimu ya Juu utaimarishwa kwa kuongeza utoaji na urejeshaji wa mikopo, ili vijana wengi zaidi waweze kufaidika na mikopo kwa ajili ya elimu ya juu.

Kuimarisha Uchumi:

Mhe. Spika, ili kuhakikisha kuwa uimarikaji wa ukuaji wa uchumi unaleta tija kwa wananchi, serikali katika mwaka 2012/13 imeweka mikakati ifuatayo:

i. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri ikiwemo barabara na viwanja vya ndege.
ii. Kuimarisha upatikanaji wa zana za kilimo, mbegu bora na mbolea kwa wakulima, sambamba na uimarishaji wa zao la karafuu.
iii. Kuendeleza kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama pamoja na miundombinu ya maji machafu.

Kuhifadhi Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi:

Mhe. Spika, sote tunashuhudia mabadiliko makubwa yanayoendelea duniani kwetu kutokana na “mabadiliko ya tabia nchi”. Miongo tulioizoea imebadilika sana, haitabiriki na imebadilisha pia mwenendo wa maisha yetu.

Athari kamili za mabadiliko hayo bado hazijulikani, ingawa imethibitishwa kuwa hali ya joto duniani inapanda, kina cha maji ya bahari kinaongezeka, upatikanaji wa maji ya kunywa na mfumo wa afya nao unaweza kuathirika. Zanzibar kama nchi nyengine yoyote ile inahitaji kuwa tayari na hali hiyo na kuchukua hatua za kujihami na athari hizo.

Mhe. Spika, serikali kwa msaada wa Shirika la Misaada la Uingereza (*DIFD*) imefanya utafiti uliolenga kubainisha namna mabadiliko ya tabia nchi yanavyoweza kuathiri maendeleo ya kiuchumi nchini kwetu.

Matokeo ya utafiti huo yamesaidia katika uandaaji wa Mpango wa Zanzibar wa Kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabia nchi na Uhifadhi wa Mazingira. Kwa kuwa suala hili ni muhimu na ni mtambuka, ni wajibu wetu sote kuchukua kila juhudi kuhifadhi mazingira yetu na kukabiliana na athari hizo za mabadiliko ya tabia nchi. *(Makofi)*

MASHIRIKIANO NA SEKTA BINAFSI:

Mhe. Spika, mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi (*PPP*) ni muhimu katika kukuza miundombinu ya uchumi ambayo ni kichocheo kikubwa cha kuleta maendeleo ya nchi.

Kwa upande wa Zanzibar, mashirikiano ya Sekta ya Umma na ya Binafsi yataharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo tafauti kama vile kukuza uzalishaji wa bidhaa za viwandani, kilimo, biashara, kukuza ajira, kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii pamoja na kuongezeka kwa mapato.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/13 Serikali imekusudia kuanzisha Kitengo cha "*PPP*" katika Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa madhumuni ya:

i. Kuandaa sera ya mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na ya Binafsi.
ii. Kuandaa mkakati, mpango na muundo wa kuendeleza mashirikiano hayo.
iii. Kutoa taaluma ya dhana ya "*PPP*" kwa wadau pamoja na kuandaa midahalo (*debates*) itakayoamsha ari za mashirikiano.
iv. Kuingiza dhana ya "*PPP*" katika mipango ya wizara na taasisi za Serikali.
v. Kutekeleza lengo la nne la klasta ya kwanza ya MKUZA II linalotaka kuundwa kwa sekta binafsi imara hapa nchini.

KUIMARISHA MAENDELEO YA JIMBO:

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/13, serikali itaanza utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo baada ya hatua za matayarisho ikiwemo uundwaji wa sheria ya kusimamia mfuko huu kukamilika. Mfuko huu unachukua nafasi ya utekelezaji wa miradi midogo midogo ya wananchi, ambapo kila jimbo lilikuwa likipatiwa kiasi cha shilingi 10 milioni.

Serikali imekusudia kuimarisha maendeleo ya majimbo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo baada ya kupitishwa Sheria ya kuanzisha Mfuko huo. Jumla ya shilingi 760 milioni zimetengwa na kila jimbo litapatiwa shilingi 15 milioni mwaka 2012/13 kutoka shilingi 10 milioni mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 50, ili kusaidia juhudi za wananchi katika kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, usimamizi mzuri unahitajika kutoka kwa viongozi wa majimbo, ili kupelekea kufikia malengo yaliyokusudiwa hasa katika Mkakati wetu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Ni imani ya serikali kwamba matumizi ya fedha hizo zitafuata taratibu zote za manunuzi kama zinavyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha na Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali. *(Makofi)*

MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2012/13:

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/13, serikali imepanga kutekeleza jumla ya *Programs* 38 na Miradi 84 (Programu 6 na Miradi 18 ni mipya) katika Mpango wake wa Maendeleo. Kiasi cha shilingi 341.1 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa utekelezaji wa Mpango huo, ambapo serikali imekadiria kuchangia shilingi 47.9 bilioni sawa na asilimia 14 na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi 293.2 bilioni sawa na asilimia 86 ya Bajeti ya kazi za Maendeleo. Kati ya fedha zinazotoka kwa Washirika wa Maendeleo, shilingi 187.7 bilioni ni mkopo na shilingi 105.4 bilioni ni ruzuku.

Mhe. Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, Klasta ya kwanza ina jumla ya *Program* 21 na Miradi 25 itakayogharimu kiasi ya shilingi 197.9 bilioni sawa na asilimia 58 ya makadirio ya bajeti ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 18.9 bilioni sawa na asilimia 10 zinatarajiwa kutolewa na serikali na shilingi 179.0 bilioni ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 90. Aidha, mikopo ni shilingi 104.5 bilioni na ruzuku ni shilingi 74.5 bilioni.

Mhe. Spika, Klasta ya pili ya Huduma za Jamii na Ustawi inatarajiwa kutumia shilingi 117.7 bilioni sawa na asilimia 35 kugharamia utekelezaji wa Program 11 na Miradi 33. Serikali inatarajiwa kutoa shilingi 13.7 bilioni

sawa na asilimia 12 ya bajeti yote ya Klasta hii na Washirika wa Maendeleo shilingi 104.0 bilioni sawa na asilimia 88. Mkopo ni shilingi 79.9 bilioni na ruzuku ni shilingi 24.1 bilioni.

Mhe. Spika, Klasta ya Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa inatarajiwa kutekeleza Program sita na Miradi 26 yenye, jumla ya shilingi 25.4 bilioni sawa na asilimia 7 ya bajeti ya Maendeleo. Serikali inatarajiwa kutoa shilingi 15.3 bilioni sawa na asilimia 60 na Washirika wa Maendeleo shilingi 10.1 bilioni sawa na asilimia 40 ya makadirio ya Klasta ya tatu ambapo Mikopo ni shilingi 3.2 bilioni na ruzuku ni shilingi 6.9 bilioni.
Miradi Mikuu kwa Bajeti ya 2012/13:

Mhe. Spika, miradi mikuu inayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka huu wa fedha ni pamoja na kukamilisha na kuzindua Ujenzi wa Njia ya Pili ya Umeme kutoka Ras-Kiromoni hadi Fumba, Mradi wa Kuimarisha Njia za Umeme, Mradi wa Kuendeleza Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria - Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, Mradi wa kuimarisha Elimu ya lazima, Mradi wa Elimu Mbadala na Amali, Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana na Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ili kukabiliana na uhaba mkubwa wa ofisi za serikali na uchakavu wa ofisi zilizopo, serikali pia itaanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali. Fedha za Mfuko huo zitatokana na kiasi kitakachoidhinishwa na Baraza lako tukufu na fedha zitakazotokana na mauzo ya majengo makongwe ya serikali. *(Makofi)*

MAANDALIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU:

Mhe. Spika, Bajeti ni nyenzo muhimu ya kuimarisha huduma kwa wananchi na utawala bora. Serikali inaendelea na mageuzi yenye lengo la kuimarisha uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa bajeti, ili kuleta manufaa zaidi kwa wananchi. Mageuzi haya yanakusudia kuanzisha mfumo wa bajeti unaozingatia matokeo kupitia utekelezaji wa Programu.

Lengo ni kuhakikisha kuwa kila Shilingi inayoidhinishwa na Baraza hili na kutumiwa na Serikali inaleta manufaa kwa walengwa na wananchi kwa ujumla. Katika utaratibu huu, bajeti za kila Wizara au Taasisi zitaandaliwa kwa kuzingatia muundo na majukumu yake na kuandaa Programu, ambazo zitaainisha matokeo yanayotarajiwa kutokana na kutekelezwa Programu hizo.

Mhe. Spika, matayarisho ya utaratibu huo mpya wa bajeti yanaendelea vizuri. Kwa kuanzia, utaratibu huu unatekelezwa kwa majaribio ukihusisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kwa hatua ya sasa, wizara hizo zimeweza kutayarisha Muundo wa Programu na Maelezo ya programu yenye kuhusisha malengo, matokeo, viashiria, shabaha na gharama za programu. Lengo kwa mwaka huu wa fedha ni kuwasilisha maelezo hayo ya Programu kwa taarifa tu sambamba na bajeti za wizara hizo zilizo katika mfumo wa sasa.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/13, serikali itaendeleza mageuzi hayo ya bajeti kwa kuandaa muundo na maelezo kama hayo kwa wizara zote zilizobakia. Matarajio ni kwamba ifikapo mwaka 2014/15 Bajeti ya Serikali iwe inaandaliwa na kutekelezwa kwa kuzingatia mfumo huo wa Programu pamoja na uidhinishaji wa Sheria ya Matumizi.

MWELEKEO WA BAJETI 2012/13:

Muundo wa Bajeti:

Mhe. Spika, serikali inatarajia kutumia jumla ya shilingi 648.9 bilioni katika mwaka wa fedha wa 2012/13, ikiwa ni ongezeko la asilimia 38.2 kutoka shilingi 469.4 bilioni zinazotarajiwa kutumika hadi kufikia mwisho wa Juni 2012. Serikali pia inatarajia kuuanza mwaka wa fedha ikiwa na bakaa ya shilingi 5.9 bilioni.

Kwa kuzingatia uwezo wa sasa wa mapato kutokana na vyanzo vya ndani, inatarajiwa kuwa mapato ya ndani yatafikia jumla ya shilingi 280.7 bilioni na hivyo kufanya jumla ya mapato hayo kufikia shilingi 286.6 bilioni. Fedha hizo ni mjumuisho wa mapato ya Kodi na yasiyo ya kodi. Kiasi hicho cha mapato cha shilingi 286.6 bilioni kitaacha nakisi katika Bajeti ya shilingi 362.3 bilioni.

Mhe. Spika, katika mwaka huu wa 2012/13, serikali inatarajia kupokea shilingi 333.2 bilioni ikiwa ni Mikopo na Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwemo Msaada wa Kibajeti shilingi 40.0 bilioni na Mikopo na Ruzuku kwa ajili ya Programu na Miradi ya Maendeleo ya shilingi 293.2 bilioni. Fedha hizo za shilingi 333.2 bilioni zinapunguza nakisi ya Bajeti hadi kufikia shilingi 29.1 bilioni.

Mhe. Spika, ili kuziba pengo hilo la bajeti, serikali inapendekeza kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha mapato ya ndani kwa kurekebisha viwango vya kodi na ada za huduma Mbale mbali.

Kwa ujumla, hatua hizo zinatarajiwa kuingiza shilingi 13.3 bilioni, ikiwemo gawio la shilingi 2.7 bilioni kutoka Mashirika ya Serikali na hivyo kuzidi kupunguza pengo la bajeti na kufikia shilingi 15.8 bilioni. Serikali inatarajia kukopa ndani, ili kuziba pengo hilo na hivyo kuleta uwiano wa mapato na matumizi katika bajeti.

MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO:

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema, serikali inakusudia kurekebisha Sheria mbali mbali za Kodi, ili kuziba nakisi ya bajeti iliyojitokeza. Kwa kuwa sio lengo la serikali kutoza kodi itakayowaumiza wananchi, marekebisho haya yamezingatiwa kwa makini sana.

Kutokana na mazingatio hayo, serikali itaendelea na Sera yake ya kutotoza Kodi ya Ongezeko la Thamani katika vyakula muhimu, huduma za afya, huduma za usafiri, mazao ya kilimo na ufugaji kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na dhamira hiyo nzuri ya serikali ya kutoongeza kodi katika bidhaa na huduma za msingi kwa wananchi, bado tunahitaji kuchukua hatua maalum za kupunguza utegemezi katika uendeshaji wa serikali yetu.

Miongoni mwa hatua hizi zitalazimisha kuongeza kodi katika baadhi ya maeneo, ili kukidhi mahitaji yetu ya matumizi na mpango wa maendeleo. Kwa kuzingatia dhamira hizo za serikali, ili kuziba nakisi ya bajeti katika mwaka ujao wa fedha 2012/13, serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya kodi katika sheria zifuatazo:-

i. Sheria ya Ushuru wa Stempu Namba 6 ya Mwaka 1996.
ii. Sheria ya Kodi ya Hoteli Namba 1 ya mwaka 1995.
iii. Sheria ya Ada za Bandari Namba 2 ya mwaka 1999.
iv. Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli Namba 7 ya mwaka 2001
v. Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009.
vi. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya mwaka 1998
vii. Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar Namba 7 1996 na
viii. Sheria ya Mafunzo ya Amali Namba 8 ya mwaka 2006.

Mhe. Spika, sambamba na marekebisho ya sheria hizo, inapendekezwa kuzifanyia marekebisho Kanuni za Sheria kadhaa, ili kurekebisha viwango vya ada mbali mbali vilivyopitwa na wakati, ikiwemo vinavyohusu ukodishaji wa ardhi kwa wawekezaji.

SHERIA YA USHURU WA HOTELI

Kurekebisha kiwango cha kodi katika huduma za mahoteli, mikahawa na kutembeza wageni

Mhe. Spika, msingi mmoja muhimu wa kutoza kodi ni kuhakikisha kuwa mfumo wa kodi unakuwa na usawa wa kulipa kodi. Kwa bahati mbaya, kumekuwa na malalamiko kuwa utaratibu wa sasa, wa kutoza kiwango cha asilimia 18 kwa Wafanyabiashara waliosajiliwa chini ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na asilimia 15 kwa wenye mahoteli, mikahawa na watembeza wageni wasiosajiliwa na Kodi hiyo, haufuati msingi huo muhimu. Ili kurekebisha kasoro hiyo, inapendekezwa kuongeza kiwango cha Kodi kwa Mahoteli, Mikahawa na Watembeza Wageni wasiyosajiliwa kwenye VAT kutoka asilimia 15 ya sasa hadi asilimia 18. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato kwa jumla ya TZS 1.96 bilioni.

Mhe. Spika, hatua hii ya kuleta uwiano wa viwango vya kodi itasaidia katika maeneo mengine kadhaa muhimu yakiwemo haya yafuatayo:

i. Kuhamasisha wafanyabiashara kujiunga kwa hiari kwenye mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

ii. Kuongeza uwajibikaji wa kuweka na kutunza kumbukumbu za mauzo ambazo ni muhimili muhimu katika kulipa kodi inayostahili.
iii. Kuimarisha ushindani miongoni mwa walipakodi zilizorekebishwa na wale wa VAT.

SHERIA YA USHURU WA STEMPU

Marekibisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu

Mhe. Spika, moja ya Sheria ambayo viwango vyake ni vidogo na vimekaa bila ya kufanyiwa marekebisho kwa muda mrefu ni Sheria ya Ushuru wa Stempu. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Stempu katika maeneo matatu ya Sheria hii kama ifuatavyo:

Kubadilisha kiwango cha utozaji wa ushuru wa stempu kwenye mikopo

Mhe. Spika, Serikali imepokea na kuzingatia malalamiko kuhusu wakopaji, hususan wawekezaji kutakiwa walipie Ushuru wa Stempu kwa asilimia moja ya thamani ya mkopo. Ushuru huu umelalamikiwa kukwaza kukua kwa huduma za fedha kwa upande mmoja na uwekezaji rasilimali kwa upande mwengine. Matokeo ya mambo haya ni kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu. Imebainishwa pia kuwa kuendelea kutozwa ushuru huu kwa asilimia ya thamani ya mkopo kunaathiri ushindani na nchi jirani. Ili kuondoa kasoro hiyo, Serikali inapendekeza kuweka ukomo wa kiwango cha juu cha kutoza Ushuru wa Stempu katika mikopo. Hatua hii haikusudii kuongeza mapato bali itasaidia kushajiisha uwekezaji biashara nchini sambamba na kuimarisha uwezo wa Zanzibar kiushindani (*competitiveness*) na usawa wa kodi miongoni mwa wakopaji.

Kurekebisha kiwango cha Ushuru wa Stempu kwa biashara

Mhe. Spika, biashara zisizofikia kiwango cha mauzo cha kusajiliwa kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani pamoja na zile ambazo hazimo katika usajili wa mfumo wa ulipaji wa Kodi wa Hoteli hutozwa Ushuru wa Stempu kwa kiwango cha asilimia moja na nusu kwa mauzo yanayoanzia thamani ya TZS 1,000. Tofauti ya kiwango hichi na kile cha VAT ni kubwa sana. Inapendekezwa kuongeza kiwango cha Ushuru wa Stempu kutoka asilimia moja na nusu ya sasa hadi asilimia tatu. Hatua hiyo itaongeza mapato ya Serikali kwa TZS 2.10 bilioni.

SHERIA YA ADA YA BANDARI

Kurekebisha na kuweka kiwango kipya cha ada ya bandari

Mhe. Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuimarisha elimu hapa nchini. Pamoja na juhudi hizo, bado Sekta ya Elimu inakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwemo upungufu wa madarasa na madawati na hivyo kuendelea kuathiri ubora wa elimu. Hatuwezi kutegemea Washirika wa Maendeleo pekee kwa kuondoa upungufu huo unaokadiriwa kuhitaji jumla ya TZS 27.0 bilioni kwa madawati peke yake. Ili kuanzisha juhudi za kupatikana fedha za kukabiliana na usumbufu huu unaowakabili watoto wetu, inapendekezwa kuongeza Ada ya Bandari kwa abiria wanaosafiri baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kutoka TZS 1,000 ya sasa hadi TZS 2,000 na kutozwa ada ya TZS 1,000 kwa abiria wanaosafiri baina ya Unguja na Pemba. Hatua hiyo inakadiriwa kuingiza jumla ya TZS 2.00 bilioni. Fedha zote zitakazopatikana kutokana na ongezeko hili la Ada ya Bandari zitatumika kwa ununuzi wa madawati tu.

SHERIA YA USHURU WA MAFUTA YA NISHATI

Kurekebisha kiwango cha Ushuru wa mafuta ya nishati

Mhe. Spika, Kwa kutambua umuhimu wa mafuta ya bidhaa za petrol kiuchumi na kijamii, Serikali imekuwa ikichukua hadhari katika marekebisho ya viwango vyake vya kodi. Kwa kuwa viwango vya Kodi hii ni maalum (specific) na havitegemei thamani ya bidhaa na kwa kuwa viwango vya sasa vya kodi vimekuwepo kwa muda mrefu bila ya kurekebishwa, kwa sasa vimepoteza thamani yake. Kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali inakusudia kurekebisha kidogo kiwango cha Ushuru wa Mafuta ili kupunguza athari ya upotezaji wa thamani bila ya kuleta athari kwa mfumko wa bei kwa wananchi. Inapendekezwa kuongeza Ushuru wa Mafuta kwa TZS 50.00 kwa kila lita inayoingia nchini kwa mafuta ya Petroli na Dizeli tu. Hatua hii inatarajiwa kuiingizia Serikali TZS 3.3 bilioni.

SHERIA YA USAFIRI BARABARANI

Marekebisho ya viwango vya leseni ya njia

Mhe. Spika, Serikali imefanikiwa sana katika jitihada zake za kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii nchini, mojawapo ikiwa ni mtandao wa barabara. Ujenzi wa barabara una gharama kubwa sana. Tunahitaji kuzitunza ili ziweze kutuhudumia kwa kipindi kirefu zaidi kijacho. Nyingi ya barabara hizi zimejengwa kwa mkopo na tunahitaji kuihudumia mikopo hiyo. Hata hivyo, kiwango cha sasa cha ada ya Leseni ya Njia cha TZS 24,000 kwa gari kwa mwaka hakizingatii matumizi ya njia kwa aina tofauti za gari. Inapendekezwa kurekebisha kiwango cha Leseni za Njia ili kiendane na uzito wa gari au na ukubwa wa injini yake. Hatua hii inatarajiwa kuiingizia Serikali jumla ya TZS 2.1 bilioni.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, idadi ya magari nchini inaongezeka kila mwaka na hivyo kuathiri mazingira kutokana na moshi unaotoka katika magari hayo (carbon emission). Tunapaswa kuchukua hatua zaidi za kukabiliana na athari za uharibifu huo ikiwemo gharama za matibabu. Kwa mwaka ujao wa fedha, inapendekezwa kutozwa TZS 15,000 kwa kila gari kwa mwaka na TZS 3,000 kwa chombo cha moto cha magurudumu mawili au matatu. Hatua hii inatarajiwa kuingiza TZS 700 milioni. Serikali inakusudia kutumia asilimia 80 ya fedha hizo, sawa na TZS 560 milioni, kama ziada katika ununuzi wa dawa kwa ajili ya hospitali zetu wakati asilimia 20 iliyobaki sawa na TZS 140 milioni zitatumika kugharamia upandaji wa miti katika maeneo yaliyoharibiwa kimazingira kwa uchimbaji mchanga, mawe na kifusi na uharibifu wa ukanda wa pwani; kupanda Mikarafuu ili kufikia lengo la Serikali la upandaji wa mikarafuu angalau laki tano kwa mwaka; kupanda miti katika maeneo ya vianzio vya maji na kuleta haiba nzuri pembezoni mwa barabara hususan katika maeneo ya utalii.

KUREKEBISHA VIWANGO VYA ADA ZA HUDUMA MBALIMBALI

Mhe. Spika, Serikali imekuwa ikitoza ada kwa huduma zake mbalimbali katika Wizara, Idara na Taasisi zake. Serikali imesikiliza malalamiko ya muda mrefu ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kuwa vingi ya viwango vya ada hizo vimepitwa mno na wakati na vinahitaji kufanyiwa mapitio na kurekebishwa. Serikali itafanya mapitio hayo kwa Sheria na Kanuni zake na kurekebisha ada hizo. Hatua hii inatarajiwa kuiingizia Serikali jumla ya TZS 0.5 bilioni.

KUIMARISHA USIMAMIZI NA UTAWALA WA KODI

Mhe. Spika**,** mbali ya hatua za kuimarisha viwango vya Kodi, Ushuru na ada mbalimbali, hatua maalum zitachukuliwa kuimarisha uwezo wa Taasisi zetu za kodi. Kwa upande wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na hizi zifuatazo:

Kuimarisha Mfumo wa usimamizi kwa Maeneo (*Block Management System*):

Mhe. Spika, ili kusimamia kwa karibu ukusanyaji mapato katika kila eneo, TRA kwa kushirikiana na ZRB zitagawa maeneo na kuweka usimamizi wake chini ya maofisa maalum watakaokuwa na jukumu la kuhakikisha kodi inakusanywa kwa shughuli zote za kiuchumi zilizo katika eneo husika. Ugawaji huo utatumia mfumo wa Kompyuta kutokana na *database* iliyopo katika Mradi wa Matumizi Endelevu ya Ardhi (*SMOLE*) ambao taarifa zake zinatumia mfumo wa *GIS*.

Kutumia mashine (*Scanner*) katika ukaguzi wa Kontena

Mhe. Spika, Serikali inatarajia kuweka mtambo maalum (*Scanner*) wa kukagulia makontena yanayoingia nchini katika bandari ya Malindi. Mtambo huu unaotarajiwa kupatikana kwa msaada wa Serikali ya Watu wa China, utasaidia kuimarisha mapato na usalama nchini kwa kutambua vitu vinavyoingizwa na hivyo kudhibiti udanganyifu unaofanywa na baadhi ya waingizaji wa bidhaa nchini wasio waaminifu.

Kurahisisha ulipaji wa kodi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo kwa kutumia simu za mikononi

Mhe. Spika, katika miaka ya karibuni huduma za simu za mikononi zimesaidia sana katika kuimarisha huduma za fedha kwa wananchi ambao hutumia simu katika kutuma fedha na kufanyia malipo ya huduma mbali mbali. Serikali, kupitia *TRA* na kwa mashirikiano na Benki ya Watu wa Zanzibar, itaanza kutumia teknolojia hiyo ya simu za mikononi katika ulipaji kodi. Njia hii inatarajiwa kuimarisha ufanisi katika ulipaji wa kodi kwa hiari

kwa upande wa Wafanyabiashara wadogo wadogo na kuokoa muda wao na hivyo kuwapa fursa zaidi za kuendeleza biashara zao.

Marekebisho ya kiwango cha Mauzo kwa usajili wa *VAT*

Mhe. Spika, kupitia *ZRB*, Serikali pia imefanya mapitio ya kiwango cha mauzo ambacho Mfanyabiashara hutakiwa kujisajili na Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*). Lengo la mapitio hayo ni kuhakikisha kuwa kiwango hicho kinakwenda na wakati, kinasaidia kuongeza ufanisi kwa kuhakikisha kuwa wanaosajiliwa ni wale tu wenye mauzo na biashara kubwa, na kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati (*SMEs*) kupata fursa ya kukua kwanza kabla ya kuingizwa katika mfumo wa *VAT*. Kutokana na mapitio hayo, inapendekezwa kupandisha kiwango cha mauzo ambacho mfanyabiashara asiekifikia hatosajiliwa kwenye *VAT* kutoka kiwango cha sasa cha TZS 15 milioni kwa mwaka hadi kiwango cha mauzo ya TZS 30 milioni kwa mwaka.

SHERIA YA MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI

Kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali
Mgawanyo wa mapato yatokanayo na kodi ya ufundi stadi (*SDL*)

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kabla, kuwa hakuna nchi inayoweza kuendelea bila ya watu wake kuelimika vya kutosha. Katika maendeleo, elimu ya juu na ile ya mafunzo ya amali ina nafasi maalum. Hata hivyo, elimu hizi zina gharama kubwa katika upatikanaji wake.

Mhe. Spika, kwa dhamira ya kusaidia katika ugharamiaji wa elimu ya juu na mafunzo ya amali nchini, Serikali ilianzisha Ushuru wa Kuendeleza Ujuzi. Katika utekelezaji wa hilo, mahitaji ya fedha kwa kuhudumia maeneo haya mawili ya elimu nchini yamekuwa yakiongezeka kwa kasi mwaka hadi mwaka. Ili kuondoa utata uliojitokeza kuhusiana na matumizi ya Ushuru wa Kuongeza Ujuzi (SDL), Serikali itaweka utaratibu bayana wa mgao wa fedha hizo baina ya mafunzo ya amali na elimu ya juu. Inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ili asilimia 60 ya ushuru huo itumike kwa ajili ya Elimu ya Juu na asilimia 40 iliyobaki kwa Mafunzo ya Amali. Mgao huu utasaidia sana kwa maeneo yote mawili kufaidika.

Kusamehe Serikali kulipa Ushuru wa Mafunzo ya Amali

Mhe. Spika, kumejitokeza pia tatizo la kuhasibu mara mbili malipo ya Serikali katika Ushuru wa Kuongeza Ujuzi. Kwa hali ilivyo sasa, Serikali inapokea ushuru huo kutoka kwa sekta binafsi na pia kujilipa pale inapochangia. Ili kurekebisha kasoro hii, inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa kutoa msamaha kwa Serikali na Taasisi zinazotegemea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, ili kutoathiri mapato yaliyokusudiwa kwa dhamira hii, Serikali itakuwa inatenga kiasi kisichopungua asilimia 3 na kisichozidi asilimia 5 ya matumizi yake ya mishahara kwa madhumuni ya elimu ya juu na mafunzo ya amali.

SHERIA YA KAZI

Kupanga kiwango cha chini cha kutozea kodi ya *PAYE* kwa wataalamu wa kigeni

Mhe. Spika, Sheria ya Uwekezaji imetoa ruhusa kwa Wawekezaji kuajiri wageni kujaza nafasi nyeti ambazo utaalamu au ujuzi wake ni adimu kupatikana nchini. Kwa bahati mbaya, fursa hii imekuwa ikitumiwa vibaya na Wawekezaji karibu wote kwa kutoa taarifa ya kiwango ambacho ni cha chini cha mshahara wanacholipa wafanyakazi hao wageni. Matokeo ya taarifa hizo ni kuikosesha Serikali mapato yake halali. Hali hii haiwezi kuvumiliwa tena. Ili kudhibiti udanganyifu huo, Serikali kupitia Kanuni za Sheria ya Kazi Namba 3 ya Mwaka 2011 iliweka viwango vya chini vinavyokubalika kama mshahara kwa Wataalam hao wageni, ambacho ni baina USD 500 mpaka USD 1,300 kwa mwezi kutegemea na nafasi ya ajira. Imebainika kwamba bado wawekezaji hutumia viwango hivyo vya chini kama ndio viwango halisi vya mishahara kwa wafanyakazi wao hata wale wa nafasi za juu.

Mhe. Spika, Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Uwekezaji (ZIPA), Idara ya Kazi, Idara ya Uhamiaji na Mamlaka ya Mapato (TRA) inatarajia kuvipitia upya viwango hivyo na kuvirekebisha ili (1) kukabiliana na udanganyifu uliopo; (2) kuhakikisha kuwa wataalam wageni wanalipa kodi kulingana na kipato chao na (3) kuhakikisha kuwa ajira zisizo na ulazima wa kuajiriwa wageni zinabaki kwa wananchi wetu.

SHERIA YA ZIPA

Kupunguza misamaha ya kodi ya mapato (*Tax Holiday*) kwa miradi ya kibiashara.

Mhe. Spika, Serikali imekuwa ikitoa vivutio mbali mbali vya kodi na visivyo vya kodi ili kushajiisha uwekezaji nchini. Vivutio hivyo vinagusa maeneo ya uwekezaji kwa ujumla hasa mahoteli na vivutio maalum kwa maeneo huru ya uwekezaji ikiwemo miradi ya viwanda na shughuli za kibiashara. Serikali tayari imechukua juhudi kubwa za kuimarisha Miundombinu ikiwemo mfumo wa barabara, huduma za umeme na maji katika maeneo mengi ya uwekezaji. Serikali katika mwaka ujao wa fedha itafanya mapitio ya vivutio vilivyopo ili kuvirekebisha kwa kuondoa visivyohitajika tena na kuangalia haja ya kuweka vivutio vipya katika maeneo maalum kama vile miradi mikubwa na nyeti.

Mhe. Spika, Serikali pia imekusudia kuongeza vivutio zaidi katika uwekezaji wa maeneo makhsusi ya kiuchumi kama vile viwanda na ya kijiografia ikiwemo kushajiisha uwekezaji katika kisiwa cha Pemba. Kwa kuanzia, Serikali itaondoa Msamaha wa Kodi ya Mapato (*Tax Holiday*) kwa miradi mipya ya kibiashara (*trading activities*) katika Maeneo Huru ya Uwekezaji na Bandari Huru. Ili kutokuathiri taswira ya Serikali kwa Wawekezaji waliokwishawekeza, hatua hii haitahusisha Miradi ambayo imeidhinishwa na ipo nchini tayari.

SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI

Kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (*Tax Administration Procedure Act*) ya mwaka 2009

Mhe. Spika, baadhi ya Miradi ya hoteli iliyosajiliwa chini ya Sheria ya *ZIPA* na kupata msamaha wa kodi wakati wa ujenzi, imebainika kuwa baada ya kukamilika hukodishwa kwa kampuni nyengine kwa uendeshaji bila ya dhima maalum kwa malipo mbali mbali ikiwemo mapato ya Serikali. Hatua zitachukuliwa kurekebisha upungufu huu. Inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (*Tax Administration Procedure Act*) ya mwaka 2009 ili iwapo mwekezaji atakodisha ama kuteua Kampuni ya kuendesha Hoteli yake, dhamana ya masuala yote ya mapato ya Serikali itabaki kwa mmiliki wa hoteli husika. Endapo deni la kodi halikulipwa na kampuni iliokodishwa au kukabidhiwa uendeshaji, dhamana au dhima hiyo itaweza kulipwa kwa dhamana ya hoteli yenyewe.

SHERIA YA MITAJI YA UMMA

Kuasisi utaratibu wa Mashirika ya Serikali kulipa gawio kutokana na Faida

Mhe. Spika, kwa muda mrefu hakujawa na utaratibu maalum kwa Mashirika ya Serikali kuchangia katika bajeti ya Serikali tokea kusitishwa utaratibu wa zamani uliokuwa ukiyataka Mashirika kuchangia bajeti ya Serikali bila ya kujali kuwa yanapata faida au la. Kuanzia mwaka ujao wa fedha, Mashirika ya Serikali yatapaswa kulipa gawio kutokana na faida (*dividend*) inayopatikana baada ya kulipa kodi husika katika biashara zao. Hatua hiyo itaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha TZS 2.7 bilioni.
Mhe. Spika, kwa ujumla, hatua zote hizi zinatarajiwa kuimarisha ufanisi katika usimamizi wa mapato na kuiingizia Serikali TZS 13.3 bilioni.

SURA YA BAJETI BAADA YA MAREKEBISHO

Mhe. Spika, baada ya marekebisho yote hayo, katika mwaka ujao wa fedha Serikali inakadiria kukusanya jumla ya TZS 294.1 bilioni kutokana na vyanzo vya ndani sawa na asilimia 21.3 ya Pato la Taifa. Ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo ya TZS 217.1 bilioni hadi mwisho wa Juni 2012, kunajitokeza ongezeko la TZS 77.0 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 35.5. Kati ya mapato hayo, jumla ya TZS 274.1 bilioni zitatokana na makusanyo ya vyanzo vya kodi na TZS 20.0 bilioni ni mapato yasiyo ya kodi. Kati ya mapato yasiyokuwa ya kodi, TZS 1.0 bilioni ni gawio kutoka Benki Kuu, TZS 2.7 bilioni ni gawio la faida kutoka Mashirika ya Serikali na mapato ya Wizara za Serikali ni TZS 16.3 bilioni.

Mhe. Spika, kati ya TZS 274.1 bilioni zitakazotokana na kodi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) inakadiriwa kukusanya TZS 106.7 bilioni, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) inatarajiwa kukusanya TZS 146.0 bilioni na TZS 21.4 bilioni zitakusanywa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kama Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar.

MAPATO YA NJE

Ruzuku na Mikopo ya Nje

Mhe. Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2012/13 inatarajia kupata jumla ya TZS 293.2 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia programu na miradi mbali mbali. Kati ya hizo, TZS 187.8 bilioni ni mikopo na TZS 105.4 bilioni ni ruzuku. Aidha, misaada ya kibajeti (*GBS*) inatarajiwa kufikia TZS 38.1 bilioni ikiwa ni asilimia 4.5 ya misaada yote ya kibajeti itakayotolewa Tanzania katika mwaka 2012/13. Kati ya fedha hizo, TZS 28.3 bilioni ni ruzuku na TZS 9.8 bilioni ni mikopo ya kibajeti. Aidha, Serikali itatumia TZS 1.9 bilioni ikiwa ni fedha kutokana na misamaha ya madeni (*MDRI*).

Mhe. Spika, kwa kuzingatia kiwango cha matumizi, na mchanganuo wa mapato kutokana na vyanzo vyake, utegemezi wa bajeti kutoka kwa Washirika wa Maendeleo umeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 21 mwaka 2012/13 kutoka asilimia 24 mwaka 2011/12 sawa na kupungua kutoka asilimia 12 ya Pato la Taifa mwaka 2011/12 hadi kufikia asilimia 9 katika mwaka wa fedha wa 2012/13.

MATUMIZI YA SERIKALI

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/13, Serikali inatarajia kutumia TZS 307.8 bilioni sawa na asilimia 47.4 kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS 341.1 bilioni sawa na asilimia 52.6 kwa kazi za maendeleo na hivyo kufanya jumla ya matumizi kuwa TZS 648.9 bilioni.

Mambo Muhimu yanayozingatiwa katika ugawaji wa fedha za Matumizi

Mhe. Spika, kwa ujumla, kati ya mapato yote yanayotarajiwa, kuna mapato ambayo huelekezwa katika matumizi maalum kabla ya kuwa na kiwango kinachogawiwa kwa Taasisi za Serikali kwa ajili ya matumizi mengineyo ya kazi za kawaida. Kwa mwaka 2012/13, kati ya mapato yote yanayotarajiwa ya TZS 648.9 bilioni, TZS 293.2 bilioni ni kwa ajili ya utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, mapato yote ya TZS 40 bilioni kutokana na Misaada ya Kibajeti na MDRI yanaelekezwa katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo.

Mhe. Spika, tunafahamu kuwa kuna matumizi ya lazima kwa Serikali kama vile maslahi ya wafanyakazi wa sasa na waliostaafu (mishahara, kiinua mgongo na pencheni) na malipo ya deni la umma na riba yake. Kwa mwaka ujao wa fedha, matumizi ya lazima kwa kazi za kawaida yanatarajiwa kufikia TZS 200.6 bilioni. Aidha, matumizi ya TZS 2.7 bilioni yametengwa kwa matumizi maalum kama nilivyoeleza awali, ikiwemo TZS 2.0 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa madawati ya skuli na TZS 0.7 bilioni zitatumika kwa ajili ya kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira, ambapo kati ya hizo TZS 0.56 bilioni zitatumika kwa ajili ya ziada ya ununuzi wa dawa na TZS 0.14 bilioni ni kwa ajili ya upandaji miti.

Mhe. Spika, baada ya kutoa matumizi yaliyoelezwa, tunabakiwa na TZS 112.4 bilioni. Kati ya bakaa hiyo, inayoweza kugawiwa kwa matumizi ya kazi za maendeleo ni TZS 7.9 bilioni na TZS 104.5 bilioni kwa ajili ya kazi za kawaida ikiwemo matumizi mengineyo ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya fedha hizo zinazoweza kugaiwa kwa kazi za kawaida, TZS 2.3 bilioni zimepangwa kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo za kilimo. Aidha, Serikali imepanga pia kununua vifaa maalum kwa kusaidia makundi mbali mbali ya watu wenye ulemavu kama vile viti vya magurudumu, visaidizi vya kusikia kwa walemavu wa masikio na fimbo za kutembelea kwa wasioona. Kwa kuanzia, Serikali imepanga kutumia TZS 0.3 bilioni kwa kusaidia wenzetu wenye ulemavu katika mwaka ujao wa fedha. Bakaa iliyobaki ya TZS 101.9 bilioni ni kwa ajili ya maeneo mengine ya matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, ahadi ya Serikali ni kuongeza maslahi ya wafanyakazi wake kila hali ya uchumi itaporuhusu. Serikali inaelewa kuwa kipato cha wafanyakazi wake walio wengi hakilingani na mahitaji yao ya maisha. Baada ya marekebisho makubwa ya mshahara yaliyofanywa mwezi Oktoba 2011, Serikali haikusudii kupandisha kima cha chini cha mshahara mwaka ujao wa fedha. Badala yake, imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha marekebisho kulingana na mahitaji ya muundo wa utumishi (*Scheme of Service*), nyongeza za mwaka, ajira mpya za lazima na upandishaji vyeo kwa watumishi wa Umma.

Mhe. Spika, sura halisi ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2012/13 ni kama inavyoonekana katika jadweli liliopo hapo chini.

Mfumo wa Bajeti ya mwaka 2012/13

Maelezo	**Makisio** 2011/12 (TZS Bil.)	**Makisio** 2012/13 (TZS Bil.)	**Ongezeko (%)**
Mapato			
A. Mapato ya ndani	**221.24**	**294.1**	**32.9**
B. 4.5% Msaada wa kibajeti (GBS)	**30.28**	**39.9**	**32.1**
C. Dhamana za Hazina na Hati Fungani	**15.00**	**15.8**	**5.5**
D. Mikopo ya Kibenki	**1.60**	**0.0**	**-100.0**
E. Bakaa iliyoletwa	**4.00**	**5.9**	**46.7**
F. Mikopo na Ruzuku	**340.96**	**293.2**	**-14.0**
Jumla ya Mapato	**613.08**	**648.9**	**5.9**
Matumizi			
G. **Matumizi ya Kawaida**	234.18	307.8	**31.4**
i) Mishahara (Mawizara)	105.78	139.6	**32.0**
ii) Mishahara (ruzuku)	20.56	17.7	**-13.4**
iii) Matumizi mengineyo (Mawizara)	47.17	71.1	**50.3**
iv) Matumizi mengineyo (ruzuku)	13.05	26.6	**103.9**
v) Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS)	47.62	52.8	**10.9**
H. MAENDELEO	**378.90**	**341.1**	**-10.0**
i) Mchango wa Serikali	37.95	47.9	**26.3**
ii) Washirika wa Maendeleo	340.96	293.2	**-14.0**
Jumla ya Matumizi	**613.08**	**648.9**	**5.9**

Chanzo*: Ofisi ya Rais - Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo*

MAMBO MUHIMU MWAKA 2012/13

i. Sensa ya Watu na Makaazi

Mhe. Spika, mipango yote tutayoipanga na kuidhinishwa na Baraza lako tukufu inalenga katika kuwaletea maisha bora wananchi wenzetu. Kama ilivyo nchi yoyote, jamii yetu inaundwa na makundi mbali mbali yakiwemo kina mama, vijana, watoto na wazee. Kwa ujumla wake, makundi ya rika na jinsia mbali mbali ndio yanaunda idadi ya watu katika nchi yetu. Makundi yote haya yana mahitaji maalum, hivyo ni muhimu kujua, sio tu idadi halisi ya watu bali pia mgawanyo wake kwa makundi na kijiografia.

Mhe. Spika, njia inayotumika kupata taarifa hizo muhimu ni kupitia Sensa ya Watu na Makaazi, ambayo nchini kwetu hufanyika kila baada ya miaka kumi. Sensa ya mwisho ilifanyika mwaka 2002 na hivyo tayari tumetimiza kipindi cha miaka kumi. Kwa kutambua umuhimu wa kujua idadi ya watu nchini, tayari Serikali imeandaa Sensa nyengine ambayo imepangwa kufanyika tarehe 26 Agosti mwaka huu wa 2012.

Mhe. Spika, ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa tunashiriki kikamilifu katika Sensa hiyo na kuhimiza wengine ili wakaazi wote wa Zanzibar wahesabiwe. Kufanya hivyo kutarahisisha mipango ya kuwaletea maendeleo kwa mujibu wa mahitaji. Wito wangu ni kuwa ifikapo tarehe 26 Agosti mwaka huu kusiwe na mkaazi yeyote wa Zanzibar ambae hatahesabiwa, mara moja tu, kipindi cha Sensa. Ni jukumu letu viongozi, wakuu wa kaya na wananchi kuhakikisha lengo hili linatimia.

ii. Uandaaji wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania

Mhe. Spika, nchi yetu imepitia vipindi mbali mbali vya demokrasia na mageuzi yake. Leo hii tunajivunia mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kufanya maamuzi kwa njia ya kidemokrasia, kwa kudumisha umoja wetu, na kwa uvumilivu wa mawazo yanayotofautiana na ya mmoja wetu.

Kwa mara nyengine tena, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekabiliwa na mtihani mwengine muhimu na adimu katika ujenzi wa demokrasia yake. Mtihani huu ni mchakato wa uandaaji wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, sote tunafahamu kuwa Katiba ndio Sheria Kuu ya nchi; sote tunafahamu kuwa Katiba ndio Mkataba wa wananchi kwa viongozi wao na hivyo sote tuufahamu umuhimu wa Katiba. Haijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu, wananchi kupata fursa ya kushiriki moja kwa moja katika uandaaji wa Katiba wanayoitaka. Fursa iliyopo mbele yetu ni adimu na tunapaswa kuitumia vyema.

Haiwezekani kuwa wananchi wote tuna mawazo yanayofanana juu ya mustakabali wa nchi yetu. Tabaan mawazo yetu lazima yatatofautiana katika mambo mengi ya Katiba hii. Sehemu muhimu ya demokrasia ni kustahamiliana pale tunapotafautiana kimawazo na kifikra. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kuwa na fikra tofauti juu ya Muundo wa Muungano wetu, wapo wanaotaka Muundo wa Muungano uendelee na wapo wanaotaka marekebisho katika muundo wa sasa. Wote hawa wana haki na mawazo yao. Lakini ni dhahiri kuwa haiyumkiniki Katiba ikabeba mtazamo zaidi ya mmoja. Kinachotarajiwa ni kuwa Katiba ibebe na kukidhi matakwa ya wananchi walio wengi kwa kuzingatia masuala yetu ya kiuchumi, kijamii, kihistoria na kijiografia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tofauti hizo za mitazamo na kutokubaliwa mtazamo uupendao mmoja wetu au kikundi miongoni mwetu hazipaswi kuwa chanzo cha vurugu, kuvunjika kwa amani au kupotezwa kwa fursa yenyewe ya kuandaliwa Katiba mpya. Kwa mara nyengine tena, serikali inatoa wito kwa Wazanzibari wote tudumishe mila na desturi zetu za upole, ustaarabu na uvumilivu wa kisiasa, kidini na kijamii ambao Wazanzibari wamenasibishwa nao kwa karne nyingi zilizopita. *(Makofi)*

Jambo la muhimu kwa upande wetu Wazanzibari ni kuhakikisha kuwa tunajitokeza kwa wingi na tunashiriki kikamilifu katika kutoa maoni yetu kwa kujenga hoja na bila ya jazba hadi kupatikana kwa Katiba tunayoitaka. *(Makofi)*

Tayari Tume ya Kukusanya Maoni imeshaundwa na inajumuisha wajumbe kutoka pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Nachukua fursa hii kumshukuru sana Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar kwa kuwateua wajumbe ambao ni ndugu zetu, weledi kitaaluma na wenye uzoefu na maadili ya kupenda nchi yao. Ni imani yangu kuwa watakuwa nguzo kuu ya kupata maoni. *(Makofi)*

SHUKRANI:

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa umahiri wako wa kuliendesha Baraza hili katika hali ya amani na utulivu. Ni matumaini yangu kwamba busara na hekima zako zitaendelea kuongoza vyema majadiliano ya vikao vya Baraza hili. *(Makofi)*

Aidha, kwa kupitia kwako napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza, ambaye ni swahibu wangu, ndugu yangu Mhe. Hamza Hassan Juma, pia Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza lako, Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa mashauriano, maoni na miongozo katika mchakato mzima wa maandalizi ya bajeti ninayoiwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maandalizi ya bajeti hii yamehusisha wadau wengi wa ndani na nje ya serikali. Napenda kuwashukuru wote waliochangia kwa kutoa maoni pamoja na Watendaji Wakuu na wafanyakazi wa wizara mbali mbali, idara zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Asasi zisizo za Kiserikali pamoja na Sekta Binafsi. Michango yao ilisaidia sana katika kufanikisha utayarishaji wa bajeti hii. *(Makofi)*

Aidha, napenda kuwashukuru watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha miswada na nyaraka mbali mbali za sheria ambazo ni sehemu ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa upande wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, napenda kutoa shukurani za pekee kwa Katibu Mkuu wangu kipenzi ndugu Khamis Mussa Omar pamoja na Katibu Mtendaji wangu kipenzi wa Tume ya Mipango Bi Amina Khamis Shaaban na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Abdi Khamis Faki. *(Makofi)*

Aidha, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha na hatimaye leo kuiwasilisha hotuba hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kutumia fursa hii adhimu kuwashukuru kwa dhati kabisa Washirika wetu wa Maendeleo katika kuchangia maendeleo ya nchi na wananchi wetu. Kwa hakika misaada yao imekuwa ni kichocheo kikubwa cha harakati za maendeleo nchini kwetu. Washirika wa Maendeleo waliochangia bajeti ya mwaka 2012/13 ni pamoja na Canada, Cuba, Denmark, Finland, India, Ireland, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Watu wa Korea, Japani, Marekani, Misri, Norway, Oman, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uturuki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mashirika ya kimataifa yaliyojitokeza kuchangia katika bajeti yetu ya mwaka 2012/13 ni *ACBF, ACCRA, AFDB, AGRA, BADEA, CARE INTERNATIONAL, CDC, CHAI, CIDA, DANIDA, DFID, EGH, EU, EXIM Bank of China, EXIM Bank of Korea, FAO, FHI, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, IAEA, ICAP, IDB, IFAD, ILO, IMF, IPEC, JICA, JSDF, KOICA, MCC, NORAD, OPEC, ORIO-Netherlands, PRAP, SAUDI FUND, Save the Children, SIDA, UN AIDS, UN, UNDP, UNESCO, UNFPA, UN-HABITAT, UNICEF, UNIDO, US AID, WB, WHO* na *WSPA. (Makofi)*

HITIMISHO:

Mhe. Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2020, MKUZA II na Malengo ya Milenia ya 2015. Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/13, kama ilivyo kwa miaka mingine, imeandaliwa kwa kuzingatia malengo ya Mipango na Mikakati hiyo mikuu.

Mhe. Spika, taswira inayojitokeza ni kuwa pamoja na jitihada zinazochukuliwa za kuongeza mapato ya ndani, bado mahitaji yetu ya kuleta maendeleo kwa haraka yanapindukia sana uwezo wetu wa kuyahudumia. Kutokana na hali hiyo, Taasisi zote za Serikali zinalazimika kuwa makini zaidi katika kubainisha na kuteua vipaumbele, ili kukidhi gharama za utekelezaji wake kulingana na rasilimali zilizopo. Serikali itasisitiza udhibiti wa matumizi na kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa Maofisa Wahasibu wote.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima, taadhima na unyenyekevu naomba sasa Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimaye lipitishe mapendekezo juu ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2012/13, ili yawe muongozo wa utekelezaji wa shughuli za serikali kwa mwaka 2012/13.

Mhe. Spika, serikali inapendekeza mbele ya Baraza lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2012/13 kukusanya jumla ya shilingi bilioni mia sita na arobaini na nane na mia tisa na arobaini na nne milioni (shilingi 648,944 milioni) pamoja na matumizi ya shilingi bilioni mia tatu na saba na mia saba tisini na saba milioni (307,797 milioni) kwa kazi za kawaida, na shilingi bilioni mia tatu na arobaini na moja na mia moja na arobaini na saba milioni (341,147milioni) kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa niaba yenu nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuwasilisha jioni hii Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli amechukua kiasi ya masaa mawili kamili kwa ajili ya kuwasilisha bajeti hiyo.

Vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe, kwamba kwa muda wote mlikuwa watulivu kwa ajili ya kusikiliza bajeti hiyo, ili hatimaye kama alivyoomba yeye mwenyewe muipokee, muijadili, mutoe muongozo na hatimaye kuipitisha bajeti hiyo kama alivyosema.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wageni wetu mbali mbali ambao wamehudhuria. Kwa kweli niliishia kuwatambua naomba nirudie tena Waheshimiwa Mabalozi Wadogo waliopo Zanzibar kutoka India *may*

excellence please rise to salute the members, the Consul General from India, inaonekana ameshaondoka. Ndugu yetu Balozi Mdogo kutoka Msumbiji namuomba asimame kama yupo, inaonekana naye amedharurika.

Waheshimiwa Wajumbe, tumemkaribisha Mhe. Balozi Mdogo wa China, ambaye ni ndugu yetu, mama yetu the *excellence please could you rise to salute the members*, inaonekana na yeye amepata dharura. Pia ndugu yetu Balozi Mdogo wa Misri, yupo pale sawa na ahsante karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Mabalozi Wadogo wa Heshima kutoka Sweden, Norway and Finland *could you please rise to salute the members, the excellences*, inaonekana wamedharurika.

Tulimkaribisha pia ndugu yetu Balozi Mdogo wa heshima kutoka Ujerumani, *could you the excellence please stand up the General Consul from German*, inaonekana hayupo, lakini hata hivyo tunashukuru.

Country Director of UNDP please rise to salute the members, pia naye hakuhudhuria. Balozi Mdogo wa heshima wa Uingereza ambaye yupo nchini *could you the excellence General Consul from Great Britain, please could you rise to salute the members*, inaonekana hayupo.

Balozi Mdogo wa heshima ambaye yupo Zanzibar kutoka Marekani, *could the excellence please rise to salute the members, if is present*, inaonekana pia hakuhudhuria.

Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kuwakaribisha pia na kuwatambua kuwepo kwa Naibu *Governor* wa Benki Kuu, yule pale ndugu yetu. Vile vile nitambue kuwepo kwa Mkurugenzi Mkaazi wa Benki Kuu ambaye yupo hapa Zanzibar, yule pale. *(Makofi)*

Pia naomba kutambua kuwepo kwa Naibu Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa ambaye yupo hapa Zanzibar, inaonekana amepata dharura, hata hivyo nashukuru.

Naomba kumkaribisha na kumtambua kuwepo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa *PBZ*, naona kumekuwa na dharura kama Mwakilishi wake yupo basi tunamkaribisha sana. Kamishna wa *TRA* ambaye yupo hapa Zanzibar kama yupo namuomba asimame kwa ajili ya kumtambua, inaonekana amepata dharura. Lakini hapana shaka ndugu yetu Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, naomba ndugu yetu asimame, yule pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kutambua kuwepo kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi Zanzibar na kama yupo namuomba asimame, inaonekana amepata dharura.

Lakini nategemea sana Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar anaweza kuwa amepata nafasi ya kuhudhuria kwa sababu tulimkaribisha pia, inaonekana hayupo. Mwenyekiti wa Kamisheni ya Mamlaka ya Mji Mkongwe kama yupo, inaonekana hayupo. Tulimualika pia Mstahiki Meya wa Manispaa ya Zanzibar, yupo. Pia Mkurugenzi wa *ZSSF*, inaonekana amepata dharura. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe tunao Wenyeviti mbali mbali wa Kamisheni, tulimuomba afike Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, inaonekana hakuhudhuria. Mwenyekiti wa *Zanzibar Chamber of Commerce*, yule pale karibu sana. *(Makofi)*

Vile vile wapo Viongozi mbali mbali wa Vyama vya Siasa akiwemo Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Magharibi, inaonekana hakuhudhuria. Pia tulimkaribisha lakini kwa nafasi yake nadhani hakuweza kuhudhuria Katibu Mkuu wa CUF kwa nafasi yake nyengine yeye ni mmoja kati ya Viongozi Wakuu hakuweza kuhudhuria. *(Makofi)*

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, inaonekana hakupata nafasi. Lakini wapo Manaibu Makatibu Wakuu wa Vyama vya Siasa kutoka NCCR, CHADEMA, TLP, UDP, TADEA, UMD, NLD, CHAUSTA pamoja na SAU kwa pamoja nawaomba wasimame, wale pale. *(Makofi)*

Wapo Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa waliopo hapa Zanzibar akiwemo kutoka *UNDP, UNFPA, UNICEF, WHO, ILO* nawaomba kama wapo wasimame, wale pale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tunaye Meneja wa *ZANTEL* ambaye tulimualika, inaonekana amepata dharura, lakini kuna Mwenyekiti wa *ZATUC* pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Zanzibar kama wapo nawaomba wasimame, wale pale. *(Makofi)*

Siku ya leo ya Hotuba ya Bajeti pia yupo Kamishna za *ZRB*, inaonekana amepata dharura. Lakini yupo Mhasibu Mkuu wa SMZ namuomba asimame, inaonekana amepata dharura. Nawakaribisha na kuwatambua waandishi wa habari na wengine wamo ndani humu na wote tunawakaribisha. *(Makofi)*

Bila ya kuwasahau watendaji mbali mbali waliohudhuria ambao sikuweza kuwataja kwa pamoja tunawakaribisha sana katika Kikao au Mkutano wetu wa Bajeti siku ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe pamoja na waalikwa nakushukuruni sana kwa kuwa watulivu kwa muda wote wa bajeti wakati ilipokuwa ikiwasilishwa na Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kwa hivyo, mpaka hapa tulipofika nimeambiwa kwamba mara baada ya shughuli hii kuna dhifa kidogo hapo nje.Waheshimiwa Wajumbe sote pamoja na wageni waalikwa mbali mbali waliohudhuria tunaombwa kujumuika hapo nje mara baada ya kumaliza shughuli zetu hivi punde.

Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutumia Kanuni ya 94(5) atoe utaratibu juu ya shughuli yetu hii.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ameshawasilisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 na kwa hivyo kukamilisha shughuli zetu za leo.

Vile vile kwa kuwa Kanuni ya 94(5) ya Baraza la Wawakilishi inaruhusu kuahirisha shughuli za Baraza kwa siku mbili, ili kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wajumbe kuisoma na kuitafakari hotuba hii ya bajeti.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuahirisha shughuli za Baraza la Wawakilishi kwa siku mbili, ili tuweze kukutana tena hapa siku ya Jumatatu tarehe 18/06/2012 saa 3:00 za asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri kuahirisha shughuli zetu hizi kwa muda usiozidi siku mbili za kazi wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kidemokrasia Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa tatu walitaka tuendelee na kazi hii kuanzia hivi sasa. Nawashukuru kwa kutumia demokrasia yao.

Waheshimiwa Wajumbe, nirudie tena kuwashukuru na mnakaribishwa sana katika dhifa ndogo hapo nje.

Baada ya hayo sasa naahirisha kikao hichi hadi siku ya Jumatatu, tarehe 18/06/2012 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 12:20 jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 18/06/2012 saa 3:00 asubuhi)